


YALIYOMO

UTANGULIZI 3

1. Maelezo ya Jumla 3
2. Umuhimu wa Sera 3
3. Uandaaji wa Sera 5
4. Muundo wa Sera 5
5. Nyenzo za Utekelezaji wa Sera 5

SEHEMU I: USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA MAJI 6

1. MAELEZO YA JUMLA 6
 - 1.1 Upatikanaji wa Rasilimali za Maji 6
 - 1.2 Kupunguka kwa Rasilimali za Maji 7
 - 1.3 Mfumo wa Sasa wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji 7
2. MAJI NA MAENDELEO YA TAIFA KIUCHUMI NA KIJAMII 7
 - 2.1 Matumizi ya Nyumbani 7
 - 2.2 Mifugo 8
 - 2.3 Kilimo 8
 - 2.4 Viwanda 8
 - 2.5 Madini 9
 - 2.6 Nishati 9
 - 2.7 Uvuvi 9
 - 2.8 Mazingira 9
 - 2.9 Wanyamapori na Utalii 10
 - 2.10 Misitu na Nyuki 10
 - 2.11 Usafirishaji katika Maji 10
 - 2.12 Maji ya Kimataifa 10
3. CHANGAMOTO KATIKA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA MAJI NA MISINGI YA SERA 11
 - 3.1 Changamoto katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji 11
 - 3.2 Umuhimu wa Kuwa na Usimamizi wa Pamoja wa Rasilimali za Maji 11
 - 3.3 Misingi ya Sera katika Kusimamia Rasilimali za Maji 12
4. MASUALA YA SERA KUHUSU USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA MAJI 13
 - 4.1 Ugawaji na Matumizi ya Maji kwa Shughuli za Kijamii na Kiuchumi 14
 - 4.2 Hifadhi ya Maji, Udhhibiti wa Ubora wa Maji na Kuzuia Uchafuzi 15
 - 4.3 Maji na Mazingira 17
 - 4.4 Tathmini, Mipango na Maendeleo ya Rasilimali za Maji 17
 - 4.5 Takwimu na Taarifa 18
 - 4.6 Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia 19
 - 4.7 Mafunzo na Maendeleo ya Watumishi 19
 - 4.8 Kujikinga na Majanga 20
 - 4.9 Maji ya Kimataifa 21
 - 4.10 Mfumo wa Kitaasisi 22
 - 4.11 Mfumo wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji 24
 - 4.12 Kugharamia Usimamizi wa Rasilimali za Maji 24



SEHEMU II: HUDUMA YA MAJI VIJIJINI 26

1. MAELEZO YA JUMLA 26

2. MADHUMUNI 26

3. MISINGI 26

3.1 Misingi ya Kijamii 27

3.2 Misingi ya Kiuchumi 27

3.3 Misingi ya Mazingira 27

3.4 Misingi ya Huduma Endelevu 27

4. MASUALA YA SERA KUHUSU HUDUMA YA MAJI VIJIJINI 28

4.1 Ushirikishaji wa Jamii 28

4.2 Kushirikisha Sekta Binafsi katika Kutoa Huduma ya Maji Vijijini 29

4.3 Jukumu la Sekta ya Umma katika Udhhibiti, Uwezesaji na Uratibu wa Sekta ya Maji Vijijini 30

4.4 Kiwango cha Chini cha Utoaji Huduma ya Maji Vijijini 30

4.5 Maji kwa Ajili ya Mifugo 30

4.6 Uvunaji wa Maji ya Mvua 31

4.7 Kuunganisha Huduma za Maji, Usafi wa Mazingira na Elimu ya Afya 31

4.8 Mwamko wa Kijinsia 31

4.9 Udhhibiti wa Utoaji Huduma ya Maji Vijijini 32

4.10 Kugharamia Miradi ya Maji Vijijini 32

4.11 Taratibu za Uendeshaji Miradi Kisheria 33

4.12 Mfumo wa Kitaasisi 33

4.13 Uratibu na Ushirikiano 34

4.14 Ufuatiliaji na Tathmini 34

SEHEMU III: HUDUMA YA MAJISAFI NA MAJITAKA MIJINI 35

1. MAELEZO YA JUMLA 35

2. MADHUMUNI 35

3. MISINGI 35

4. MASUALA YA SERA KUHUSU MAJISAFI NA MAJITAKA MIJINI 36

4.1 Vyanzo vya Maji na Miundombinu ya Maji 36

4.2 Uwekezaji na Ulipaji Maji 37

4.3 Udhhibiti wa Matumizi ya Maji 38

4.4 Maji kwa Wakazi Wenye Kipato Kidogo 39

4.5 Majitaka na Mazingira 39

4.6 Mfumo wa Kitaasisi 40

4.7 Mfumo wa Kisheria 40

4.8 Sekta Binafsi 41

4.9 Ubinafsishaji wa Huduma ya Majisafi na Majitaka Kwenye Miji Midogo 41

4.10 Ufuatiliaji na Tathmini 42

4.11 Uwajibikaji kwa Umma 42

4.12 Kujenga Uwezo 42

4.13 Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia 43

4.14 Uratibu na Ushirikiano 43

Ramani ya Mabonde ya Mito, Tanzania 44

UTANGULIZI

1. Maelezo ya Jumla

Maji ni muhimu kwa viumbe vyote duniani, bila maji hakuna uhai. Aidha maji ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kiwango cha maendeleo ya jamii yoyote kinategemea kuwepo kwa maji ya kutosha na yenye ubora unaotakiwa. Katika hali yake ya asili, maji ni sehemu ya mazingira ambapo wingi na ubora wake ndio unaosaidia katika kuamua jinsi maji yatakavyotumika. Upatikanaji wa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na usafi wa mazingira ni muhimu katika kulinda afya za wananchi. Utumiaji wa maji ambayo sio salama na uhaba wa maji huchangia katika kusababisha milipuko na kuenea kwa magonjwa kama kuhara na kipindupindu. Japokuwa maji ni muhimu kwa uhai wa viumbe, na maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hakuna uwiano wa mgawanyo wa maji ulio sawa kati ya sehemu moja na nyingine na katika majira mbalimbali ya mwaka. Aidha, wingi wa maji yanayofaa kwa matumizi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi una kikomo, na maji hayo pia yanaweza kuathirika kirahisi.

Maji yanayofaa yanaendelea kupungua siku hadi siku kutokana na kuongezeka kwa mahitaji. Mathalan, katika kipindi cha miaka 15 iliyopita, mahitaji ya maji yameongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na ongezeko la watu nchini, ongezeko la uzalishaji mali katika sekta mbalimbali hususan kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji umeme, uzalishaji viwandani, utalii, uchimbaji madini, ufugaji, uvuvi, matumizi kwa ajili ya usafi wa mazingira na mahitaji ya maji kwa ajili ya wanyamapori. Aidha, upungufu wa maji unasababishwa na uharibifu wa mazingira, hali inayosababisha vyanzo vingi vya maji kukauka au kupungua. Pia, upungufu wa maji hutokana na ukosefu au upungufu wa mvua katika baadhi ya maeneo hapa nchini na matumizi mabaya ya maji hayo. Upungufu huu unaathiri uzalishaji wa chakula na umeme na kusababisha uharibifu wa mazingira, hali inayoleta migogoro na ushindani wa kutumia maji miongoni mwa sekta mbalimbali za kijamii na zile za kiuchumi. Matatizo mengine katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji hapa nchini yapo katika maeneo ya utunzaji wa rasilimali za maji katika Mabonde ya kimataifa, masuala ya sheria na mfumo wa kitaasisi wa kusimamia kikamilifu rasilimali za maji nchini. Aidha, tatizo lingine linalokabili rasilimali za maji ni kuwepo kwa mipango tofauti ya kuendeleza na kusimamia rasilimali hizi ambayo inafanyika katika misingi ya kimkoa na kiwilaya bila kuzingatia hali halisi ya rasilimali za maji zilizopo katika Mabonde husika.

Pamoja na jitihada za Serikali za kuendeleza huduma za maji kuanzia miaka ya 1970, kiwango cha upatikanaji wa huduma hizo sio cha kuridhisha. Lengo la Sera ya Maji ya 1991 lilikuwa kuwapatia wananchi wote maji safi na salama katika umbali usiozidi mita 400 ifikapo mwaka 2002. Utekelezaji wa lengo hili unaonesha kuwa karibu 50% ya wananchi walio vijijini ndio wanaopata huduma hiyo. Kiwango halisi ni chini ya hapo, kwani zaidi ya 30% ya miradi iliyojengwa vijijini haifanyi kazi vizuri kutokana na hali duni ya matengenezo na uendeshaji. Kwa upande wa huduma ya maji mijini, ni 73% ya wakazi wake ndio wanaopata huduma hiyo. Hata hivyo, kutokana na mitambo ya kusafishia maji katika baadhi ya miji kuchakaa na kukosa matengenezo, hali inayosababisha kutofanya kazi ipasavyo, hali ya ubora wa maji yanayopatikana sio ya kuridhisha.

2. Umuhimu wa Sera

Katika kipindi cha zaidi ya miaka kumi tangu Sera ya Maji ilipotangazwa rasmi mwaka 1991, kumekuwepo na mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi na kijamii, yenye mwelekeo wa kushirikisha wananchi, Sekta Binafsi, na Halmashauri za Wilaya na za Miji, na kupungua kwa majukumu ya Serikali Kuu katika uendeshaji na utoaji wa huduma za jamii. Kwa mfano, mwaka mmoja baada ya Sera kupitishwa, mwaka 1992, nchi yetu iliweka sahihi kukubali kutekeleza Azimio la Rio kuhusu mazingira, hii ikiwa ni pamoja na kulinda rasilimali za maji dhidi ya uchafuzi.



Upungufu mkubwa katika Sera Maji ya mwaka 1991 upo kwenye mikakati ya utekelezaji wa malengo yaliyoainishwa, kwani Sera ililenga zaidi Serikali Kuu kuwa mwekezaji, mwendeshaji na msimamizi wa miradi ya maji vijijini na mijini, na mtunzaji wa rasilimali za maji. Upungufu mwingine ni kuhusiana na hifadhi ya rasilimali za maji na mazingira, suala ambalo halikupewa umuhimu unaostahili.

Sababu ya msingi ya kuwa na Sera hii ni kuweka mfumo madhubuti na endelevu wa kuendeleza na kusimamia kikamilifu rasilimali za maji hapa nchini. Hii ni pamoja na kuandaa na kutekeleza taratibu za kisheria na kuweka muundo wa kitaasisi wenye uwezo wa kutekeleza Sera hii. Sera inalenga kuwashirikisha kikamilifu walengwa wa huduma za maji katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na kubuni, kupanga, kujenga, kuendesha na kufanya matengenezo ya miradi ya maji na pia kuchangia gharama za utoaji wa huduma hizo. Sera pia, inalenga kutatua matatizo ya maji katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi, utunzaji na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji na ushirikishaji wa wadau wote katika kusimamia rasilimali za maji hapa nchini. Sera hii itasaidia pia kuweka misingi endelevu ya kusimamia na kuendeleza kikamilifu rasilimali za maji katika hali ya mabadiliko ya kiutendaji hasa baada ya Serikali kupunguza majukumu ya moja kwa moja ya kutoa huduma hizo na kubakia na majukumu ya kuratibu, kushauri, kuwezesha, kusimamia na kutoa miongozo.

Maji na Dira ya Taifa 2025

Dira ya Taifa ya Mwaka 2025 inalenga kuinua hali ya maisha ya wananchi na kuwa na utawala bora unaozingatia Sheria na uchumi imara. Pamoja na mambo mengine, Dira ina malengo makuu yafuatayo:

- (i) Maisha bora yaliyo endelevu katika mazingira huru, yasiyokuwa na kukithiri kwa umaskini.
- (ii) Utawala bora unaozingatia Sheria.
- (iii) Uchumi imara, endelevu na wenye manufaa kwa wote.

Ili kufanikisha malengo ya Dira ya Taifa ya 2025 ya kufuta umaskini, kuwa na chakula cha kutosha na cha uhakika, afya bora na kuwa na bayoanuai endelevu, maji ni moja ya nyenzo muhimu katika kufikia malengo haya. Sera ya Maji na mapitio ya mifumo ya kisheria na ya kitaasisi inalenga la kufanikisha Dira hii.

Maji na Mkakati wa Kitaifa wa Uondoaji Umaskini

Mkakati wa Kitaifa wa Uondoaji Umaskini umebaini malengo ya muda wa kati na vigezo vya kupimia maendeleo ya azma hii. Ifikapo mwaka 2010 mkakati huu umejiwekea malengo makuu yafuatayo:

- (i) kupunguza umaskini kwa ukuaji wa uchumi wenye usawa.
- (ii) kuboresha maisha na uwezo wa wananchi kijamii.
- (iii) kuzuia uduni wa maisha miongoni mwa maskini.

Ni muhimu vilevile kuzichukulia rasilimali za maji kama kiungo muhimu kati ya uzalishaji na usalama wa chakula na ustawi wa mazingira na bayoanuai. Kutokana na kiwango cha maji kwa kila mwananchi kuzidi kupungua kadiri idadi ya watu inavyoongezeka, upo umuhimu wa kuongeza ufanisi wa uzalishaji wa chakula kwa kutumia maji kidogo. Lililo muhimu zaidi ni kuwa na mizania sahihi ya matumizi ya maji, mahitaji ya maji na kiasi cha maji kilichopo. Kwa kuwa maji ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hapana budi kuandaa mikakati madhubuti ya kusimamia rasilimali hiyo ili iweze kutoa msukumo unaostahili kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Taifa.



3. Uandaaji wa Sera

Sera hii imeandaliwa kwa kushirikisha kikamilifu wadau mbalimbali katika sekta ya zinazohusiana na maji hapa nchini. Wadau muhimu katika ngazi mbalimbali za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji walishirikishwa kutoa maoni na ushauri wao kwenye makongamano na mikutano mbalimbali katika ngazi za Taifa, Mkoa na Wilaya. Rasimu ya Sera hii ilipitiwa kwa kina na vyombo mbalimbali vikiwemo wizara, taasisi, vyuo na mashirika yasiyo ya kiserikali.

4. Muundo wa Sera

Sera hii imegawanyika katika maeneo makuu matatu kama ifuatavyo:

- (i) Usimamizi wa rasilimali za maji,
- (ii) Utoaji wa huduma ya maji vijijini, na
- (iii) Utoaji wa huduma ya majisafi na majitaka mijini.

Sera kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji inalenga kuweka na kuendeleza mfumo endelevu na madhubuti wa kusimamia rasilimali za maji hapa nchini, kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Sera kuhusu huduma ya maji vijijini, inalenga kuboresha afya za wananchi waishio vijijini na kuchangia katika kupunguza umaskini uliokithiri kwa kutoa huduma endelevu ya maji safi, salama na ya kutosha. Kuhusu huduma ya majisafi na majitaka mijini, Sera inalenga kuweka mfumo endelevu wa kutoa huduma hiyo kwa ufanisi na kwa bei nafuu ili kuwezesha makundi yote ya jamii yaishio mijini yafaidike na huduma hiyo. Aidha, mbali na Sera yenyewe, mipango na mikakati mahsusi ya kuitekeleza itaandaliwa.

5. Nyenzo za Utekelezaji wa Sera

Nyenzo zifuatazo zitatumika katika utekelezaji wa Sera hii:

- (i) Nyenzo za Kiufundi: Nyenzo hizi ni pamoja na hatua ambazo hutumika kudhibiti matumizi ya maji zikiwemo ujenzi wa milango ya maji, mita za maji, na matumizi ya teknolojia zisizoathiri mazingira.
- (ii) Nyenzo za Kiuchumi: Nyenzo hizi ni pamoja na bei za maji, ada za kutumia maji, faini na vivutio vitakavyotumika kukuza biashara ya maji na kutoa changamoto katika kupunguza matumizi mabaya ya maji na kupunguza uchafuzi wa vyanzo vya maji. Nyenzo hizi zitasaidia pia katika ugawaji wa maji.
- (iii) Nyenzo za Kiutawala: Nyenzo hizi ni pamoja na mifumo ya usimamizi na utoaji wa taarifa mbalimbali, mipango ya rasilimali za maji, ikiwemo mipango ya kuhifadhi vyanzo vya maji, vielelezo mbalimbali juu ya mifumo ya rasilimali za maji na miongozo kuhusu rasilimali za maji.
- (iv) Nyenzo za Kisheria: Nyenzo hizi ni pamoja na udhibiti utakaosimamiwa na chombo cha kisheria na Serikali. Hii ni pamoja na leseni za kuchukua maji kutoka kwenye vyanzo, na mapitio yake, miongozo, vibali vya kumwaga majitaka, maadili ya utoaji huduma za maji, viwango, tathmini za athari za mazingira, na makubaliano na mahusiano ya kimataifa kuhusu rasilimali za maji ya kimataifa.
- (v) Nyenzo za Udhibiti: Nyenzo za udhibiti ni pamoja na vyombo sahihi vya usimamizi wa Mabonde katika ngazi zote za Mabonde pamoja na miongozo mbalimbali. Aidha, miongozo na taratibu hizi zinajumuisha utoaji wa vibali, taratibu za wazi za utoaji hati za haki za utumiaji maji na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji.
- (vi) Nyenzo ya Ushirikishaji: Nyenzo hizi zinajumuisha uhamasishaji, elimu kwa umma, ushauri na majadiliano.



SEHEMU I: USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA MAJI

1. MAELEZO YA JUMLA

1.1 Upatikanaji wa Rasilimali za Maji



Pamoja na kwamba karibu 70% ya dunia imefunikwa na maji, ni 2.5% tu ya maji hayo ni maji baridi. Asilimia sabini ya maji baridi yapo kwenye mifumo ya barafu iliyopo Arctic, Antartica na Greenland. Kiasi cha maji baridi yaliyobakia (30%) ni maji yanayojumuisha unyevunyevu uliopo kwenye udongo, na maji chini na juu ya ardhi. Theluthi moja tu ya maji haya ndio yanapatikana katika mito, maziwa na katika kina kifupi chini ya ardhi na hivyo kuweza kutumiwa na binadamu.

Aidha, kiasi cha maji yote ya mito duniani (kilomita za ujazo 42,700) yakigawanywa na idadi ya watu billion 5.85 kwa mwaka 1995, wastani wa maji kwa kila mtu kwa mwaka ulikuwa mita za ujazo 7,300. Kufuatana na ongezeko la watu, kiasi hiki cha maji kimepungua kwa 37% tangu mwaka 1970.

Hapa Tanzania, kiasi cha maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu na kinachopatikana kwa sasa ni kilomita za ujazo 89 sawa na mita za ujazo 2,700 kwa mtu kwa mwaka. Kufuatia ongezeko la watu nchini kutoka milioni 33 mwaka 2001, hadi milioni 59.8 ifikapo mwaka 2025, kiasi hiki cha upatikanaji wa maji kwa mtu kwa mwaka kitapungua kwa 45% na kufikia mita za ujazo 1,500, ikiashiria kwamba wakati huo patakuwepo na uhaba wa maji, kwani kiasi cha maji chini ya mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka ni kiwango kinachoonesha kuwa kuna uhaba wa maji.

Rasilimali za maji zilizopo hapa nchini ni mito, maziwa, maeneo oevu na maji chini ya ardhi. Zaidi ya nusu ya nchi inapata wastani wa mvua chini ya milimita 800 kwa mwaka. Hali ya hewa aina ya monsoni huambatana na mabadiliko makubwa ya mvua mwaka hadi mwaka, na hivyo kusababisha mabadiliko makubwa zaidi ya mitiririko ya mito. Takwimu za wastani wa mvua zinaonesha kuwa maeneo ya Mashariki ya Pwani yanapata mvua zaidi ya milimita 1,000 kwa mwaka na sehemu kame zinapata mvua chini ya milimita 600 kwa mwaka. Mvua za wastani wa milimita 1,200 hadi 2,600 kwa mwaka, zinapatikana katika maeneo ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi; milima ya Kilimanjaro, Meru, Uluguru, Ukaguru na Usambara; na pia sehemu kubwa ya Magharibi ya nchi. Sehemu hizi zina mito inayotiririka kwa mwaka mzima. Katika maeneo mengine ya nchi kukosekana kwa mvua za uhakika (chini ya milimita 800 kwa mwaka) kunasababisha mito kuwa na maji kwa kipindi kifupi tu katika mwaka.

Maji mengi hupatikana kwenye maziwa ambayo yana jumla ya eneo la kilomita 60,000 za mraba. Ziwa Tanganyika ambalo lipo Magharibi mwa nchi, linapakana na nchi za Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Zambia. Ziwa hili ni la kwanza kwa kuwa na kina kirefu na ufukwe mrefu barani Afrika na ni la pili kwa kuwa na kina kirefu duniani. Ziwa Victoria, chanzo muhimu cha Mto Nile na la pili kwa ukubwa duniani, linapakana na nchi za Kenya, Uganda na Tanzania. Ziwa Nyasa ambalo lipo Kusini mwa nchi, linapakana na nchi za Malawi na Msumbiji, na lipo kwenye mfumo wa Bonde la Mto Zambezi.

Upatikanaji wa maji chini ya ardhi unatofautiana kulingana na jiolojia na hali ya hewa. Karibu 75% ya nchi ina miamba migumu chini ya ardhi, lakini pale ambapo ina nyufa na mipasukopasuko inakuwa na uwezo wa kuhifadhi maji chini ya ardhi. Aina nyingine ya miamba inayohifadhi maji ni ile yenye asili ya chokaa na ile yenye asili ya mchanga. Visima vilivyochimbwa katika maeneo ya ukanda wa Pwani ambapo kuna miamba yenye asili ya chokaa na mchanga, vina uwezo wa kutoa maji ya kiasi cha mita za ujazo 50 kwa saa. Aidha,



sehemu za Kaskazini na Kusini mwa nchi zenye miamba aina ya volkano ni nzuri kwa upatikanaji wa maji chini ya ardhi. Visima vilivyochimbwa katika maeneo hayo hutoa maji hadi kiasi cha mita 800 za ujazo kwa saa. Katika maeneo kadhaa, maji chini ya ardhi yana chumvi nyingi na madini ya aina ya fluoride, kwa matumizi ya binadamu. Maji chini ya ardhi ndio chanzo cha majisafi na ya nyongeza katika sehemu nyingi nchini. Aidha, maji hayo ndio chanzo cha uhakika kwa ajili ya matumizi mbalimbali katika sehemu kame nchini.

1.2 Kupunguka kwa Rasilimali ya Maji

Upungufu wa rasilimali ya maji na ongezeko la mahitaji ya rasilimali hiyo huathiri uwekezaji uliofanywa katika miradi inayotegemea maji, na hivyo kusababisha migogoro miongoni mwa watumiaji wa maji. Katika baadhi ya sehemu, upanuzi wa maeneo ya umwagiliaji hasa wakati wa kiangazi husababisha kukauka kwa mito, na pia huathiri bayoanuai na maisha ya wanyamapori. Matumizi mabaya ya maji, kama vile ufanisi mdogo wa umwagiliaji katika miradi mingi (unaokadiriwa kuwa kati ya 10% na 15%); na upotevu wa maji katika mifumo ya usambazaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, unaokadiriwa kufikia 52%, na ambao unasababishwa na kuvuja kwa mabomba ya maji, huchangia kuwepo kwa upungufu wa maji.

1.3 Mfumo wa Sasa wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji

Mfumo wa sasa wa usimamizi na matumizi ya rasilimali za maji unasimamiwa na Sheria ya Matumizi na Usimamizi ya Maji Na. 42 ya mwaka 1974 na marekebisho yake. Sheria ya Marekebisho Na.10 ya mwaka 1981 ilihusisha masuala ya uhibitaji wa uchafuzi wa rasilimali za maji. Hata hivyo, Sheria ya Matumizi ya Maji na Sheria nyingine zinazohusiana na maji, hazikidhi changamoto mpya za usimamizi wa rasilimali za maji zinazojitokeza nchini.

Ili kuweza kusimamia, kupanga na kuendeleza rasilimali za maji, nchi imegawanywa katika Mabonde tisa (tazama ramani). Mabonde hayo ni: (i) Pangani, (ii) Wami/Ruvu, (iii) Rufiji, (iv) Ruvuma na Pwani ya Kusini, ambayo yote yanamwaga maji yake kwenye Bahari ya Hindi, na (v) Ziwa Nyasa, (vi) Ziwa Rukwa, (vii) Ziwa Tanganyika, (viii) Ziwa Victoria, na (ix) Bonde la Bubu, na Maziwa ya Eyasi na Manyara. Usimamizi wa Mabonde ya maji ni mlolongo wa masuala na shughuli mbalimbali kuanzia kwenye vidakio vya maji hadi fukwe za bahari.

2. MAJI NA MAENDELEO YA TAIFA KIUCHUMI NA KIJAMII

Maji ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Binadamu anahitaji maji ya kunywa ili aishi, na pia kwa ajili ya matumizi yake mengine ya nyumbani. Aidha, maji yanahitajika katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile uzalishaji viwandani, umwagiliaji mashamba, ufugaji, usafishaji wa madini, uzalishaji wa umeme, usafiri na uchukuzi, burudani na utalii.

2.1 Matumizi ya Nyumbani

Idadi ya watu kwa sasa inakadiriwa kuwa milioni 34, ambapo 80% kati yao wanaishi vijijini. Inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2025 idadi ya wakazi nchini itaongezeka kwa karibu mara dufu, ambapo 60% kati yao wataishi vijijini. Ongezeko hili litaathari upatikanaji wa huduma ya majisafi na majitaka na usafi wa mazingira kama hatua madhubuti hazitachukuliwa. Hivi sasa 73% ya wakazi wa mijini wanapata huduma ya maji, wakati ambapo kwa vijijini ni 50%. Hii inadhihirisha kuwa huduma ya maji bado si ya kuridhisha. Mathalan, katika sehemu kame za katikati ya nchi, upatikanaji wa maji hata kwa ajili ya usafi wa mwili tu, bado ni tatizo kubwa. Wananchi, hasa wanawake na watoto hutembea umbali mrefu kutafuta maji. Uchumi wa nchi unaathirika kwa kukosekana kwa huduma ya maji ya kutosha mijini na vijijini.



2.2 Mifugo

Mwaka 2000 mifugo ilichangia takriban 13.3% ya mchango wa Sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa ambao ni 48.2%. Asilimia 40 ya kaya za wakulima wa vijijini wanajihusisha na kilimo na ufugaji. Mifugo pia ni chanzo cha nguvu kazi katika kilimo na usafirishaji. Mifugo mingi ipo katika maeneo kame, ambayo yana uwanda wa nyasi kavu au mbuga na mvua kidogo kwa kilimo. Tabia ya kuhamahama na idadi kubwa ya mifugo inasababisha migogoro ya maji na ardhi baina ya wafugaji na watumiaji maji wengine. Uhaba wa malisho na sehemu za kunyweshea mifugo, hususan wakati wa kiangazi, husababisha misongamano mikubwa ya mifugo katika maeneo machache yenye malisho na maji, hivyo kuathiri rasilimali za maji na mazingira. Suala muhimu katika sekta hii ni jinsi gani mifugo itapewa maji ya kutosha na ya uhakika ili kupunguza migogoro na kuongeza mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa.

2.3 Kilimo

Madhumuni makubwa ya Sera ya Taifa ya Kilimo ni kuhakikisha kuwa kunakuwepo na chakula cha kutosha katika ngazi ya taifa na kaya. Mwaka 2000 Sekta ya Kilimo ilichangia 48.2% ya Pato la Taifa. Tanzania ina kiasi cha hekta milioni 43 za ardhi inayofaa kwa kilimo. Kati ya enelo hilo, ni hekta milioni 6.3 tu zinazolimwa ambazo ni sawa na 15% ya ardhi inayofaa kwa kilimo. Hivi sasa Sekta ya kilimo inategemea kilimo cha mvua ambacho kinaathiriwa na ukame kutokana na mvua zisizo za kutosha wala za uhakika.

Kilimo cha umwagiliaji ni kinga dhidi ya ukame, pia ni njia muhimu ya kuhakikisha kuwepo kwa akiba ya kutosha ya chakula. Vilevile, kilimo cha aina hii kinachangia kuondoa umaskini kwa vile watu wengi wanaweza kulima mazao yenye bei kubwa kama vile mbogamboga na matunda. Inakadiriwa kuwa Tanzania ina eneo la hekta milioni moja linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kati ya eneo hilo, ni hekta 150,000 tu ndizo zinazolimwa hivi sasa. Karibu 80% ya eneo hili hulimwa kwa njia ya umwagiliaji wa asili ambao huchangia katika upotevu mkubwa wa maji. Eneo lilobaki (20%) lipo chini ya mashamba makubwa ya umwagiliaji yanayomilikiwa ama na serikali, taasisi au watu binafsi. Katika Bonde la Mto Pangani, kwa mfano, mazao ya chakula yanayolimwa kwa njia ya umwagiliaji ni migomba, maharage, na mahindi; wakati mazao ya biashara ni maua, mpunga na kahawa. Kilimo cha umwagiliaji kinatumia maji mengi na hivyo kuathiri upatikanaji wa rasilimali za maji kwa matumizi mengine. Kwa mfano, katika Mabonde ya mito Pangani na Rufiji, mashamba ya umwagiliaji yapo upande wa juu wa mitambo ya kuzalishia umeme, hivyo kusababisha sekta hizi mbili kushindana katika matumizi ya maji yaliyomo katika mfumo wa mto mmoja. Aidha, shughuli za kilimo zinachangia katika uchafuzi wa maji kutokana na matumizi ya madawa ya kilimo na mbolea ambayo hatimaye huyeyuka na kuingia kwenye mikondo ya vyanzo vya maji wakati wa kipindi cha mvua.

2.4 Viwanda

Sekta ya viwanda ilichangia 8.3% ya Pato la Taifa mwaka 1999 na 8.4% mwaka 2000. Aidha, mwaka 2000 Sekta hii ilikua kwa 4.8% ikilinganishwa na 3.6% mwaka 1999. Ongezeko la mchango na kukua kwa sekta ya viwanda linatokana na ukarabati wa viwanda vilivyobinafsishwa na uanzishwaji wa vingine vipya. Uzalishaji viwandani hutegemea, miongoni mwa mambo mengine, uhakika wa upatikanaji wa huduma ya maji. Kwa kuzingatia matarajio ya kukua kwa uchumi kati ya 1995 – 2025, mahitaji ya maji pia yataongezeka. Mchango wa Sekta ya viwanda katika Pato la Taifa unategemewa kuongezeka zaidi ya mara tatu ifikapo 2025.

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inalenga kuubadilisha uchumi wetu kutoka ule unaotegemea kilimo chenye tija ndogo kwenda kwenye uchumi wa kisasa unaotegemea viwanda, na kuongeza mchango wa Sekta ya viwanda katika Pato la Taifa. Kwa ajili hiyo, maji ya kutosha



na ya uhakika yanahitajika ili kuikuza sekta ya viwanda. Hata hivyo, upo uwezekano wa uchafuzi na uharibifu wa rasilimali za maji kutokana na ongezeko la viwanda endapo majitaka na takataka nyingine kutoka viwandani vitaruhusiwa kuingia kwenye mikondo ya vyanzo vya maji bila kusafishwa.

2.5 Madini

Sekta ya Madini ni muhimu katika uchumi wa nchi na inakua kwa kasi. Dira ya sekta ya madini kwa miaka 25 ijayo ni kuwa na Sekta Binafsi ambayo ni imara. Mashirika ya umma ya uchimbaji madini yamebinafsishwa na wawekezaji binafsi wamefunguliwa milango chini ya utaratibu wa biashara huria. Hivyo, Sekta ya Madini imevutia wawekezaji wengi wa nje. Wachimbaji binafsi wamo katika makundi muhimu wawili:- wachimbaji wadogo wadogo; wengi wao wakiwa ni wazalendo, na wachimbaji wakubwa, wengi wao wakiwa ni wa kutoka nje.

Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa uliongezeka kutoka 2.1% mwaka 1999 hadi 2.3% mwaka 2000. Aidha, mwaka 2000 Sekta hii ilikua kwa 13.9% ikilinganishwa na 9.1% kwa mwaka 1999. Ongezeko hili limetokana na juhudi za Serikali za kutoa vivutio na mazingira mazuri kwa wawekezaji wakubwa na wadogo.

Majukumu mapya ya Serikali ni kuendelea kuipa msukumo Sekta ya Madini ili iendeleo kukua kwa kasi; ikiwa ni pamoja na kuhamasisha na kuendeleza wawekezaji wadogo vijijini. Umuhimu unawekwa kwenye uchimbaji salama usioathiri mazingira katika migodi mikubwa na midogo. Maji mengi yanahitajika wakati wa usafishaji wa madini na hatimaye kuzalisha maji machafu yatokanayo na shughuli za usafishaji wa madini, ambayo yakimwagwa ovyo huathiri mazingira.

2.6 Nishati

Zaidi ya 60% ya umeme unaozalishwa hapa nchini unatokana na nguvu ya maji. Upo pia uwezekano wa kuzalisha umeme katika Mto Mara na Mto Kagera. Hata hivyo, uendelezaji wa mito hiyo unahitaji makubaliano na nchi shiriki. Japokuwa maji mengi hayapotei katika njia hii ya uzalishaji umeme, kwani baada ya uzalishaji maji hurudishwa kwenye mkondo wake, tatizo lililopo ni kwamba, mabwawa mengi ya kuzalisha umeme yamejengwa sehemu ambazo ni kame na hivyo upotevu wa maji kwa njia ya mvukizo ni mkubwa. Kwa mfano, upotevu wa maji kwa njia hiyo kwenye mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu ni zaidi ya 30% ya maji yanayoingia kwenye mabwawa hayo. Vyanzo vya maji kwa ajili ya uzalishaji wa umeme unaotokana na nguvu ya maji vitaendelezwa hasa katika Bonde dogo la Mto Kilombero, Mto Rufiji na Ziwa Nyasa. Masuala muhimu katika Sekta ya Nishati ni usimamizi wa mabwawa, migogoro ya watumiaji maji waliopo juu na chini ya mabwawa hayo, na athari katika mazingira.

2.7 Uvuvi

Tanzania imebahatika kuwa na rasilimali nyingi zitokanazo na uvuvi katika maji chumvi na maji baridi. Sekta ya uvuvi ina mchango mkubwa kijamii na kiuchumi. Sekta hii inachangia katika kuondoa umaskini, kuongeza akiba ya chakula na upatikanaji wa ajira. Mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa kwa mwaka 2000 ulikuwa 2.7% wakati ambapo mwaka 1999 ulikuwa 2.6%. Masuala muhimu katika sekta hii ni upatikanaji wa maji ya kutosha na yenye ubora unaofaa.

2.8 Mazingira

Kiasi cha maji kinachopita katika mto kwa ajili ya mazingira na kina cha maji ni muhimu sana kwa ajili ya bayoanuai, maeneo oevu na fukwe za bahari. Upungufu wa maji katika mito husababisha viumbe hai waishio majini kupungua kwa sababu ya kupungua hewa ya oksijeni



na virutubisho vilivyomo kwenye maji. Majitaka yatokanayo na matumizi ya maji mijini, kama hayakusafishwa huchafua maji chini na juu ya ardhi. Aidha, matumizi ya maji yasiyozingatia matumizi mengine husababisha uharibifu wa mazingira. Kwa mfano, viumbe hai katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha (Bonde la Mto Rufiji) wanaathirika kutokana na upungufu wa maji katika Mto Ruaha Mkuu unaosababishwa na kilimo cha umwagiliaji wakati wa kiangazi katika Uwanda wa Usangu.

Maeneo mengi hapa nchini ni oevu ama kwa mwaka mzima, au kwa kipindi fulani cha mwaka. Maeneo haya pamoja na maeneo ya mafuriko yana jumla ya eneo la hekta milioni 2.7 ambayo ni mazalio ya viumbe hai ambavyo ni muhimu katika hifadhi ya mazingira. Pia, maeneo haya yana viumbe hai adimu ambavyo vipo hatarini kutoweka. Maeneo oevu ni muhimu katika shughuli za utalii, uvuvi, na uwindaji. Aidha, maeneo hayo yanasaidia katika kupunguza athari za mafuriko, mmomonyoko wa ardhi, kujaa kwa tope kwenye mifereji na mabwawa. Pia, maeneo hayo husaidia katika matumizi ya virutubisho na kuboresha hali ya hewa. Maeneo ambapo mito huingia baharini ni muhimu kwa mazalio ya viumbe hai vya majini, utalii, na burudani.

2.9 Wanyamapori na Utalii

Maeneo yenye wanyamapori ni 28% ya eneo la Tanzania; kati ya eneo hilo 19% ni mbuga za wanyama ambapo hakuna watu wanaoishi. Katika sehemu nyingine binadamu huishi katika maeneo yenye wanyamapori. Wanyamapori huchangia karibu 2% ya Pato la Taifa.

Utalii ni mojawapo ya sekta zenye uwezo mkubwa wa kuchangia kukua kwa uchumi wa taifa. Kwa mfano, nchi yetu ina ufukwe wa bahari ulio safi wenye urefu wa kilomita 804. Pia, kuna maporomoko mazuri ya maji, mabonde, mito mikubwa, chemichemi za maji ya moto na hifadhi za taifa ambazo zinatoa burudani za kuvutia. Upungufu wa maji katika mito kadhaa wakati wa kiangazi huathiri maisha ya wanyamapori, na hivyo kuathiri utalii na uchumi wa nchi kwa ujumla.

2.10 Misitu na Nyuki

Tanzania ina karibu eneo la hekta milioni 33.5 za misitu. Karibu theluthi mbili ya eneo hilo ni mbuga ambayo ina ardhi inayoathirika kutokana na uchomaji moto na ongezeko la shughuli za kilimo, ufugaji na shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi. Misitu ni makazi ya viumbe hai na hutoa mchango mkubwa katika hifadhi ya rasilimali za maji. Sekta ya misitu na ufugaji wa nyuki ilichangia 3% ya Pato la Taifa katika mwaka 2000.

2.11 Usafirishaji katika Maji

Tanzania haina mito mingi inayoweza kutumika kwa ajili ya usafiri. Hii inatokana na tofauti kubwa ya miinuko iliyopo kutoka pwani hadi bara. Hata hivyo, mito kama Rufiji, Kilombero, Kagera na Malagarasi inatumika kwa usafirishaji kwa kiasi fulani. Pia, kuna mito kadhaa ambayo ina sehemu za vivuko ambavyo vinahitaji maji mengi na kina cha kutosha. Aidha, usafiri unafanyika katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika kutumia vyombo vya usafiri upo uwezekano wa umwagaji mafuta na takataka nyingine majini na hivyo kuathiri ubora wa maji.

2.12 Maji ya Kimataifa

Tanzania inashirikiana na nchi jirani katika kumiliki rasilimali za maji ya kimataifa. Rasilimali hizo zinajumuisha Maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa, Chala na Jipe; pamoja na mito ya Kagera, Mara, Umba, Ruvuma na Songwe. Kila Ziwa au Mto una tabia yake ya kihidrolojia, matatizo na changamoto zinazotofautiana katika usimamizi na uendelezaji wake. Baadhi ya matatizo na changamoto hizo ni pamoja na masuala ya mazingira kama vile uchafuzi wa



vyanzo vya maji, mambo yahasuyo utunzaji wa bayoanuai, uhifadhi wa maji na maeneno oevu, menejimenti ya samaki katika vyanzo vya kimataifa, na kuzuia magugu maji. Aidha, masuala mengine yanahusu mipango ya uendelezaji wa miradi ya umwagiliaji, maji kwa matumizi ya nyumbani na mifugo, na uzalishaji umeme. Yapoa pia masuala ya kuimarisha mipaka ya nchi ambayo ni mito au maziwa, kurekebisha matumizi yake na kuhamisha maji kutoka Bonde moja kwenda Bonde jingine. Ili kuweza kutumia kikamilifu maji ya kimataifa, juhudi zinapaswa kuelekezwa kwenye kufahamu mahitaji halisi ya Tanzania na kuwa na mipango ya kitaifa, na ya ushirikiano na nchi husika.

3. CHANGAMOTO KATIKA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA MAJI NA MISINGI YA SERA

3.1 Changamoto katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji

Ujenzi wa miradi na matumizi ya rasilimali za maji unatakiwa kuwa endelevu ili kukidhi mahitaji ya maji ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Katika kufanya hivyo itazingatiwa kuwa:

- (i) Maji kwa ajili ya mahitaji ya msingi ya binadamu yanakuwepo, ili kuleta ustawi wa jamii, na akiba ya maji ya kutosha kwa ajili ya hifadhi ya mazingira,.
- (ii) Maji kwa ajili ya uzalishaji wa chakula, umeme na shughuli nyingine za kiuchumi yanakuwepo.
- (iii) Viwango vya ubora wa maji vinafuatwa bila kuathiri hifadhi ya rasilimali hii; kuhakikisha kuwa shughuli za usimamizi wa rasilimali za maji zinagharimiwa; viwango vya ada za matumizi ya maji vinapangwa na mapato yanatumika katika usimamizi wa rasilimali za maji.
- (iv) Usimamizi wa rasilimali za maji unatekelezwa kwa pamoja kulingana na mahitaji mbalimbali.
- (v) Kuwepo kwa mikakati madhubuti ya kutatua matatizo ya matumizi ya rasilimali za maji.
- (vi) Kunakuwepo ushirikishaji wa walengwa wote katika mipango na maamuzi ya uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji.
- (vii) Takwimu za rasilimali za maji zinakuwepo na zinapatikana kwa urahisi kwa wote, na kuwa miundombinu ya kukusanyia takwimu inakuwepo na inafanya kazi.
- (viii) Kunakuwepo mfumo imara wa kitaasisi utakaotatua migogoro inayohusu rasilimali za maji.
- (ix) Kunakuwepo wataalamu wa kutosha.

3.2 Umuhimu wa Kuwa na Usimamizi wa Pamoja wa Rasilimali za Maji

Katika kuzingatia masuala na matatizo ya usimamizi wa rasilimali za maji, upo umuhimu wa kuwa na usimamizi wa uwiano wa rasilimali za maji ili kuhakikisha kuwa maji hayawi kikwazo katika maendeleo ya taifa. Mtazamo mpya ni kuwa na “Nchi ambapo kuna usimamizi endelevu wa rasilimali za maji kwa maendeleo ya jamii, uchumi na kwa mahitaji ya mazingira”. Utaratibu wa sasa una mtazamo wa kisekta, hauhusishi sekta mbalimbali katika kupanga matumizi kwa pamoja. Utaratibu huu umetokana na mtazamo wa maendeleo ya kimkoa na hauweki mkazo katika uimarishaji wa miundo ya usimamizi wa rasilimali za maji. Aidha, utaratibu kama huo unalenga kuendeleza rasilimali za maji na sio kuhifadhi na kusimamia rasilimali hizo, na unalenga kwenye udhibiti usioshirikishi kama nyenzo muhimu ya utekelezaji wa Sera. Mfumo kamilifu unazingatia ushirikishaji, unaziunganisha sekta mbalimbali katika usimamizi wa maji, unatambua kuwa maji ni rasilimali yenye ukomo, unazingatia uhusiano wa matumizi ya ardhi na maji, na unatambua nafasi muhimu ya mfumo wa ekolojia katika uchumi wa taifa.

Kimsingi, utaratibu mpya unaonesha mabadiliko ya fikra katika maeneo makuu matatu kama ifuatavyo:



- (i) Ukamilifu: mtazamo wa pamoja unaunganisha sekta mbalimbali za maji katika mipango na usimamizi unaohakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za maji.
- (ii) Uwezeshaji: maamuzi yafanywe katika ngazi ya chini kadiri iwezekanavyo, kwa kushirikisha wadau katika kupanga, kusanifu na kutekeleza maamuzi.
- (iii) Uchumi: Maamuzi katika Sekta ya Umma, Sekta Binafsi na jamii nzima katika matumizi ya maji yatazingatia thamani ya maji kadiri ya uhaba wa maji unavyoongezeka, upangaji wa bei za maji, kuchangia gharama na vivutio vingine vinavyohusu matumizi bora ya maji.

3.3 Misingi ya Sera katika Kusimamia Rasilimali za Maji

Tangu mkutano wa Umoja wa Mataifa uliofanyika Mar del Plata, Argentina mwaka 1977, mikutano mbalimbali ya kimataifa kuhusu rasilimali za maji na mazingira imekubaliana juu ya misingi ya kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji. Makubaliano ya kimataifa juu ya misingi ya Maji na Maendeleo Endelevu, Dublin, 1992; na Mkutano wa Umoja wa Mataifa juu ya Mazingira na Maendeleo uliofanyika mjini Rio de Janeiro, 1992 (Agenda 21, Sura Na. 18) ni kama ifuatayo:

- (i) Maji ni rasilimali yenye kikomo, na inayoweza kuathirika kirahisi na ni muhimu kwa maendeleo ya jamii, uchumi na mazingira.
- (ii) Uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji ufanyike kwa kushirikisha kikamilifu makundi mbalimbali katika jamii husika, hususan watumiaji maji, waandaaji wa mipango na wenye kutoa maamuzi.
- (iii) Wanawake ni watumiaji, wasimamizi na watunzaji wakuu wa maji na wanapaswa kushiriki kikamilifu katika maamuzi ya matumizi ya maji hayo.
- (iv) Maji yana thamani katika matumizi yake yote ikiwa ni pamoja na mazingira.

Kutokana na uzoefu uliopatikana hapa nchini na nchi nyingine, misingi ifuatayo itatumika katika kusimamia kikamilifu rasilimali za maji:

- (i) Matumizi ya maji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii
 - Maji ni rasilimali inayotumiwa na wote, hivyo matumizi yake yataamuliwa kulingana na sheria na taratibu zilizowekwa.
 - Mfumo wa ugawaji wa maji utabainisha na kutenganisha hati ya haki ya kutumia maji na umiliki wa ardhi.
 - Maji ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya binadamu na kwa ajili ya usafi wa mazingira ni mahitaji ya msingi.
- (ii) Kulinda na Kuhifadhi Rasilimali za Maji
 - Kanuni ya “Mchafuzi wa rasilimali za maji kutakiwa kulipa fidia ya uchafuzi kulingana na kiwango cha uchafuzi” itatumika.
 - Ufanisi na hifadhi ya maji katika aina zote za matumizi utawekewa mkazo.
 - Njia za kudhibiti mahitaji zitatumika sambamba na matumizi ya maji.
- (iii) Maji na Mazingira
 - Shughuli za kuendeleza rasilimali za maji zilenge kuboresha mazingira au kupunguza athari za uharibifu wa mazingira.
 - Mgao wa maji kwa ajili ya hifadhi ya mazingira utambuliwe na kupewa umuhimu unaostahili.
 - Maji kwa ajili ya mahitaji ya mazingira yatatambuliwa kwa kutumia taarifa sahihi za kisayansi kwa kuangalia viwango vya mahitaji katika vipindi tofauti vya mwaka kwa lengo la kulinda na kuhifadhi ikolojia ya Bonde husika.
- (iv) Kupanga na Kuendeleza Rasilimali za Maji



- Mabonde ya mito, makubwa na madogo, yatakuwa ndiyo maeneo ya kufanyia tathmini ya kupanga na kusimamia rasilimali za maji.
 - Mipango inayohusu rasilimali za maji itashirikisha wadau wote, na pia sekta mbalimbali husika.
 - Mipango itazingatia mahitaji yote ya bayoanuai na afya ya jamii.
- (v) Taarifa, Elimu na Mawasiliano
- Taarifa na kumbukumbu, ikiwa ni pamoja na takwimu kuhusu maji juu na chini ya ardhi (wingi na ubora) na takwimu kuhusu mambo ya kijamii na kiuchumi, zinahitajika ili kusaidia katika kuchukua hatua zinazostahili, kwa shughuli zote zinazohusiana na maji.
 - Elimu ni muhimu kuhusu miradi yote ya maji, ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakuwa endelevu na yenye manufaa kwa afya ya jamii.
 - Mawasiliano na upashanaji taarifa ni nyenzo muhimu katika ngazi zote za usimamizi wa rasilimali za maji.
- (vi) Maji ya Kimataifa
- Ushirikiano wa aina zote kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji ya kimataifa utazingatia misingi ya usawa na haki na kwa uwiano unaofaa.
 - Ushirikiano katika uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji ya kimataifa utaimarishwa.
 - Ushirikiano wa kiufundi, na hasa kwenye nyanja za utafiti, ukusanyaji wa takwimu na kupeana taarifa, utapewa msukumo. Hii itahakikisha kuwa wawakilishi halali wa wadau wanashirikishwa ili mfumo wa uwakilishi uwajibike kikamilifu.
- (vii) Mfumo wa Kitaasisi
- Taratibu za kiutawala na za utoaji maamuzi zitawekwa ili kuhakikisha panakuwepo usimamizi wa pamoja wa rasilimali za maji katika Mabonde.
 - Majukumu ya kusimamia rasilimali za maji, na usimamizi wa sheria, ikiwa ni pamoja na kuweka viwango vya utunzaji endelevu wa rasilimali za maji, yatatenganishwa kitaasisi na yale ya utoaji wa huduma.
 - Ngazi za chini zitapewa madaraka zaidi katika kusimamia rasilimali za maji, kwa kuzingatia kanuni na taratibu zitakazowekwa.
 - Masuala ya kijinsia yatazingatiwa katika hatua zote za kusimamia rasilimali za maji.
 - Majukumu na uwajibikaji wa Serikali na uongozi katika ngazi zote yatafafanuliwa kwa uwazi na maeneo ya uwajibikaji yatabainishwa na kuwa rasmi.
 - Muundo na mfumo wa usimamizi wa rasilimali za maji utaandaliwa ili kurahisisha ushirikishaji wa mamlaka zote katika ngazi mbalimbali.
 - Ushirikishaji wa vyombo vya watumiaji maji pamoja na Sekta Binafsi ni suala la msingi.
 - Taasisi mbalimbali zinazosimamia rasilimali za maji, ikiwa ni pamoja na makundi shiriki katika ngazi zote, zitawezeshwa na kuimarishwa.
 - Mfumo wa usimamizi wa rasilimali za maji utakuwa wa uwazi na wenye kuwajibika kwa umma.

4. MASUALA YA SERA KUHUSU USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA MAJI

Madhumuni ya usimamizi wa rasilimali za maji ni kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za maji kwa manufaa ya wananchi kwa kufuata misingi iliyowekwa.

Madhumuni mahsusi ya usimamizi wa rasilimali za maji ni:

- (i) Kuweka utaratibu wa haki ya kuyafikia maji na ugawaji wa rasilimali za maji.
- (ii) Kuhakikisha kuwa shughuli za huduma za jamii na sekta za uzalishaji, na mazingira zinapata mgao wake kulingana na mahitaji.
- (iii) Kuhakikisha kuwa maji yanatumika kikamilifu na kwa ufanisi.



- (iv) Kuweka msukumo katika usimamizi wa ubora na hifadhi ya rasilimali za maji.
- (v) Kuboresha usimamizi na hifadhi ya mifumo ya ekolojia na maeneo oevu.
- (vi) Kuweka msukumo katika kupanga na kusimamia rasilimali za maji kwa pamoja.
- (vii) Kuhamasisha wananchi na kupanua wigo wa ushirikishaji wa wadau katika kupanga na kuendeleza rasilimali za maji.
- (viii) Kuhakikisha kuwa vyombo vya kusimamia maji kimabonde vinatekeleza majukumu yake na panakuwepo uhuru wa kufanya maamuzi yake na kujiendesha vyenyewe kimapato.
- (ix) Kuendeleza ushirikiano wa kimataifa katika kupanga na kusimamia rasilimali za maji.
- (x) Kuweka msingi wa kuandaa mfumo wa usimamizi wa kitaasisi na kisheria kwa ajili ya kusimamia rasilimali za maji.

4.1 Ugawaji na Matumizi ya Maji kwa Shughuli za Kijamii na Kiuchumi

4.1.1 Maji kama Rasilimali ya Umma

Lengo: Kuwa na utaratibu wa haki ya kuyafikia maji na ugawaji wa rasilimali za maji ili sekta zote za kijamii na kiuchumi ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Rasilimali za maji katika nchi yetu ni muhimu kwa uhai na maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Uzalishaji mali katika sekta zote hutegemea upatikanaji wa maji kwa kiwango na ubora unaostahili. Maji ni muhimu katika kujihakikishia hifadhi ya chakula, matumizi ya nyumbani na usafi wa mazingira, maendeleo ya mifugo, uzalishaji umeme, uzalishaji viwandani, uvuvi na kwa mahitaji ya wanyamapori na mazingira. Rasilimali hii pia hutumiwa kama njia rahisi ya kutupia na kusafisha takataka mbalimbali kutoka viwandani, mijini na mashambani. Ni dhahiri kuwa maji ni rasilimali ya umma yenye thamani kubwa. Ili kuilinda na kuifanya iwe endelevu inahitaji kutunzwa na kuhakikisha kuwa inatumiwa kwa ufanisi, na kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Sheria na taratibu zitawekwa ili kuhakikisha kuwa, kama zilivyo rasilimali nyingine za taifa, kikatiba na kisheria, mmiliki mkuu wa rasilimali ya maji nchini kote ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwamba kila mwananchi anayo haki sawa ya kutumia rasilimali hii kwa manufaa yake na Taifa.

4.1.2 Kipaumbele Katika Matumizi ya Maji

Lengo: Kuwa na kipaumbele katika kugawa maji ili kuhakikisha kuwa shughuli za huduma za jamii, mazingira na uzalishaji zinapata mgao wake kulingana na mahitaji kwa kuzingatia rasilimali zilizopo, na kuziwezesha kuongeza tija, na pia kuepusha migongano.

Maji yanayofaa yanaendelea kupungua siku hadi siku kutokana na kuongezeka kwa mahitaji. Mathalan, katika kipindi cha miaka 15 iliyopita mahitaji ya maji yameongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na ongezeko la watu nchini, ongezeko la uzalishaji mali katika sekta mbalimbali hususan kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji umeme, uzalishaji viwandani, utalii, uchimbaji madini, ufugaji, uvuvi na matumizi na kwa ajili ya usafi wa mazingira na mahitaji ya maji kwa ajili ya wanyamapori. Aidha, upo upungufu wa maji unaosababishwa na uharibifu wa mazingira, hali inayosababisha vyanzo vingi vya maji kukauka au kupungua, na kuvifanya visiweze kukidhi mahitaji. Upungufu wa maji pia hutokana na kiwango kidogo cha mvua katika baadhi ya maeneo hapa nchini na hivyo kuvifanya vyanzo vingine vya maji kama mito, mabwawa n.k kutokuwa na maji ya kutosha. Haya yote huathiri upatikanaji wa maji kwa matumizi ya nyumbani, uzalishaji wa chakula na umeme na hifadhi ya mazingira, hali inayosababisha migogoro na ushindani wa kutumia maji miongoni mwa sekta mbalimbali za kijamii na za kiuchumi.



Katika kupanga matumizi ya maji, umuhimu wa kwanza ni maji ya kutosha kukidhi mahitaji ya msingi ya binadamu. Umuhimu wa pili ni maji yatakayotengwa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya mazingira, ili kulinda mfumo wa ekolojia na bayoanuai ambayo ni sehemu muhimu ya rasilimali za maji kwa sasa na siku zijazo. Matumizi mengine yatapangwa kulingana na vigezo vya kijamii na kiuchumi, ambavyo vitafanyiwa mapitio ya mara kwa mara. Matumizi ya rasilimali za maji katika Mabonde ya kimataifa yatafuata msingi wa haki na usawa wa kutumia na kutunza maji hayo kiuwiano kulingana na makubaliano yatakayowekwa. Aidha, uchukuaji wa maji na umwagaji wa majitaka kwenye vyanzo vya maji utahitajika uwe na kibali cha “haki ya kutumia maji” au “haki ya kumwaga majitaka” ambacho kitatolewa kwa muda maalum. Vibali vya kutumia maji vitatolewa kwa kuzingatia misingi ya matumizi bora ya maji. Taratibu, vigezo na miongozo ya utoaji wa vibali hivyo zitatayarishwa na kutekelezwa.

4.2 Hifadhi ya Maji, Udhhibiti wa Ubora wa Maji na Kuzuia Uchafuzi

4.2.1 Hifadhi ya Maji

(a) Matumizi endelevu na hifadhi ya rasilimali za maji

Lengo: Kuwa na misingi na taratibu za usimamizi wa ubora na hifadhi ya rasilimali za maji, pamoja na kuboresha na kulinda mifumo ya ikolojia na maeneo oevu.

Maji yapo katika mito, mabwawa, malambo, maziwa, maeneo oevu, chemichemi na chini ya ardhi. Maji haya hutumika kwa shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Pamoja na umuhimu wake, matumizi mabaya na uharibifu husababisha rasilimali hizi zisiwe endelevu na hivyo kuhatarisha mifumo ya ikolojia, afya za wananchi, uhakika wa hifadhi ya chakula, uzalishaji viwandani, na uwekezaji katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Migogoro iliyokwishajitokeza katika Mabonde ya Pangani na Rufiji ni kati ya uzalishaji umeme na kilimo cha umwagiliaji, hifadhi ya mazingira na kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji umeme na hifadhi ya mazingira, na watumiaji wa maji walio juu na wale walio chini ya vyanzo vya maji. Vilevile uchafuzi wa mazingira na vyanzo vya maji kutokana na kukua kwa miji na ongezeko la uzalishaji viwandani unachangia kupungua kwa ubora wa maji. Hali hii isipodhibitiwa rasilimali zetu zitaathirika na hivyo kuvikosesha vizazi vijavyo haki zao za msingi. Aidha, kutokuwa na mipango madhubuti ya pamoja ya matumizi ya maji miongoni mwa sekta mbalimbali, kukosekana kwa takwimu za kutosha kuhusu maji na matumizi ya maji yasiyo ya ufanisi, kunafanya tatizo hili kuwa kubwa zaidi.

Ili kuhakikisha kuwa rasilimali zetu za maji zinatumika kiuendelevu, zinahifadhiwa na kwamba mifumo ya ikolojia na bayoanuai inadumishwa mambo yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Usimamizi wa rasilimali za maji utalenga jinsi maji yatakavyotumika kwa manufaa na kwa ufanisi, na ugawaji wake kuzingatia uendelevu wa rasilimali hiyo. Aidha, uratibu, ufuatiliaji na tathmini za mara kwa mara, vitafanywa ili matatizo yaweze kubainishwa na hatua za kuirekebisha hali hiyo kuchukuliwa mapema.
- (ii) Vivutio vya kibiashara, pamoja na njia za kiutawala na kisheria zitatumika kama mojawapo ya vichocheo vya kuhifadhi maji.
- (iii) Wenye kutoa huduma za maji mijini na vijijini, wazalishaji umeme, wamwagiliaji wa maji mashambani, wazalishaji viwandani na migodini, n.k watalazimika kuongeza ufanisi wa mifumo yao ya utoaji na usambazaji maji ili kuzuia upotevu wa maji usio wa lazima.
- (iv) Pale itakapoonekana kuwa inafaa, uvunaji wa maji ya mvua, usafishaji wa majitaka ili yatumike tena, na usafishaji wa maji ya bahari utafanyika ili kuongeza wingi wa maji kwa matumizi mbalimbali.

(b) Uendelezaji Endelevu wa Rasilimali ya Maji Chini ya Ardhi



Lengo: Kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali ya maji chini ya ardhi kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Maji chini ya ardhi ni chanzo muhimu kwa matumizi ya binadamu, mifugo na umwagiliaji, viwanda, n.k. katika maeneo mengi nchini. Katika baadhi ya maeneo nchini ambayo yana uhaba mkubwa wa maji, kama vile Mikoa ya Shinyanga, Pwani, Mwanza, Arusha, Mara, Tabora, Dodoma, Singida, Mtwara na Lindi, chanzo hiki ni cha uhakika zaidi kuliko maji ya juu ya ardhi. Hivi sasa, uendelezaji wa rasilimali ya maji chini ya ardhi unafanywa bila kuwa na uhakika wa wingi na ubora wa maji yaliyopo kutokana na ukosefu wa takwimu na kutokuwa na kanuni mahsusi za uratibu na ufuatiliaji. Hali hii imesababisha baadhi ya sehemu kuwa na matumizi chini ya uwezo wa chanzo na mahali pengine kuwa na matumizi zaidi ya uwezo wa chanzo. Matumizi zaidi ya uwezo wa chanzo huleta mwingiliano wa vyanzo vilivyopo, na pia husababisha maji ya bahari kuingia kwenye miamba ya kuhifadhi maji kwa maeneo ya pwani. Aidha, Sekta Binafsi imeanza kushiriki kwa kiwango kikubwa katika uendelezaji wa rasilimali hii hasa katika kutoa ushauri wa kitaalamu, na makampuni ya kuchimba visima nayo yanajihusisha moja kwa moja na uendelezaji wa rasilimali hii. Hata hivyo hapajawekwa taratibu na miongozo iliyo kamilifu inayosimamia uendelezaji wa rasilimali hii, na hivyo kuhatarisha uendeleu wake.

Ili kuweka misingi imara ya uendelezaji na matumizi ya rasilimali ya maji chini ya ardhi mambo yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Vyanzo vya maji chini ya ardhi vitasimamiwa kwa kuzingatia mfumo wa miamba inayohifadhi maji, pamoja na mfumo wa Mabonde.
- (ii) Utaratibu wa kudhibiti uchafuzi wa vyanzo hivi utawekwa na kutekelezwa.
- (iii) Maeneo yanayochajisha maji chini ya ardhi, yenye miamba inayohifadhi maji chini ya ardhi, na yale ambayo yamo hatarini kuathirika au maji yake hayana ubora unaofaa yataainishwa, na kutambuliwa na kulindwa dhidi ya uchafuzi na uharibifu. Pale ambapo itaonekana inafaa, maeneo hayo ya vyanzo muhimu yatatengwa na kutangazwa kuwa ni maeneo ya hifadhi.
- (iv) Shughuli za tathmini, utafiti na udhibiti wa uchimbaji visima zitaimarishwa.
- (v) Taratibu, miongozo na usimamizi wa shughuli za kuendeleza rasilimali za maji chini ya ardhi ikiwa ni pamoja na kuchimba, kuendeleza na kuendesha miradi ya maji kutokana na visima zitafanyiwa mapitio na kusambazwa.

4.2.2 Usimamizi wa Ubora na Udhibiti wa Uchafuzi wa Maji

Lengo: Kuwa na rasilimali za maji zenye ubora na wingi unaotakiwa.

Uchafuzi wa rasilimali za maji umekuwa ukisababishwa na majitaka toka majumbani na madawa ya kilimo, shughuli za usafishaji wa madini, n.k. Yote hayo huchangia kupunguza ubora wa maji na kuyafanya yasiweze kutumika au kuhitaji fedha nyingi kuyasafisha. Aidha, ongezeko la shughuli za binadamu, ikiwa ni pamoja na matumizi ya ardhi, uchepuaji holela wa maji na uchafuzi wa maji unaathiri wingi na ubora wa rasilimali za maji zilizopo. Kwa kawaida uamuzi wa chanzo kipi cha maji kitumike hutegemea usafi na ubora wa maji katika chanzo hicho. Tatizo lingine ni kuwepo kwa magugu maji katika Ziwa Victoria na sehemu zingine za mito na mabwawa, kunakotokana na kuongezeka kwa virutubishi.

Ili kurekebisha hali hii maji yatalindwa dhidi ya uchafuzi kwa kuchukua hatua zifuatazo:

- (i) Tathmini za mara kwa mara za ubora wa maji zitafanyika ili kubaini hali halisi na kuchukua hatua za haraka pale ambapo ubora wa maji utaonekana kupungua.
- (ii) Masuala ya wingi na ubora wa maji yatashughulikiwa kwa pamoja.
- (iii) Utaratibu wa “mchafuzi wa maji kulipa fidia kulingana na kiwango cha uchafuzi aliousababisha” utatumiwa pamoja na hatua nyingine za kisheria na kiutawala.



- (iv) Wanaoendesha viwanda, mamlaka za miji, umwagiliaji wa mashamba makubwa na migodi watalazimika kukusanya na kuhifadhi takwimu sahihi za kiwango cha uchafu unaoingia kwenye vyanzo vya maji na kuziwasilisha kwa mamlaka husika.
- (v) Uhamasishaji wa umma juu ya umuhimu wa kutunza rasilimali za maji dhidi ya uchafuzi ikiwa ni pamoja na ule unaotokana na matumizi holela ya madawa ya kilimo utafanywa.

4.3 Maji na Mazingira

Lengo: Kuwa na usimamizi wa maji unaolinda mazingira na mifumo ya ikolojia na bayoanuai.

Maji ni muhimu katika kudumisha mfumo wa ikolojia na hifadhi ya mazingira, ambao unajumuisha maeneo oevu, uwanda wa mafuriko na milango ya mito inapoingia baharini na fukwe za bahari. Mfumo huu unafanya kazi kubwa ya kihadrolajia na ya kiikolojia kama vile kuchuja uchafu kwenye maji, kulinda viumbe hai, kudumisha mizania ya maji chumvi na maji baridi kwenye milango ya mito, n.k. Aidha, usimamizi wa mfumo huu ni sehemu muhimu ya usimamizi wa pamoja ya rasilimali za maji lakini hapajawekwa kanuni na taratibu muafaka za kuhakikisha uendeleu wa maeneo haya muhimu ya kiikolojia. Usimamizi kamilifu wa rasilimali za maji kwenye mabonde ni mlolongo wa shughuli mbalimbali zinazohusiana na maji kuanzia juu hadi fukwe za bahari. Shughuli hizi zinatakiwa kupangwa kwa uangalifu ili kuongeza ubora wa maji na kupunguza athari kwenye mazingira. Aidha, shughuli mbalimbali za matumizi ya ardhi kama vile kulima kwenye miinuko mikubwa na kukata miti kunasababisha mmomonyoko wa ardhi na huchangia ongezeko la tope ambalo hutiririka kwenye mabwawa ya maji na kupunguza ujazo wa mabwawa. Tope likiwa jingi pia huchafua maji na kufanya usafishaji wake kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kuwa wa gharama kubwa.

Ili kulinda mifumo ya ikolojia na bayoanuai ambayo kwa pamoja ni sehemu muhimu ya mfumo endelevu wa rasilimali za maji hatua zifuatazo zitachukuliwa:

- (i) Mahitaji ya maji kwa ajili ya mazingira ikiwa ni pamoja na wingi na vina vya maji kwa nyakati mbalimbali, juu na chini ya ardhi yatabainishwa kwa kutumia njia bora za kisayansi, na maji hayo yatatengwa kwa ajili hiyo.
- (ii) Ili kukabiliana na tatizo la mmomonyoko wa ardhi wananchi watahamasishwa na kuelimishwa juu ya njia bora za matumizi ya ardhi.

4.4 Tathmini, Mipango na Maendeleo ya Rasilimali za Maji

4.4.1 Tathmini ya Rasilimali za Maji

Lengo: Kuwa na msingi bora na endelevu wa kusimamia na kuandaa mipango ya matumizi ya rasilimali za maji.

Tathmini ya wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi ni msingi wa kuandaa mipango endelevu ya rasilimali za maji. Kwa ujumla, mipango thabiti haiwezi kufanyika bila tathmini ya kina kuhusu rasilimali za maji zilizopo. Tathmini hii inazingatia sekta zote katika ngazi ya bonde na taifa na inahusu ukusanyaji wa takwimu za wingi na ubora wa maji, hali yake, mahali inapopatikana na mwenendo wa matumizi, na namna ambavyo maji hayo hukidhi matumizi na matakwa ya matumiaji. Aidha tathmini hii ni pamoja na miradi kwa ajili ya matumizi ya maji na ile ya kukabiliana na majanga mbalimbali yatokanayo na maji kama vile mafuriko na ukame. Kwa sasa mfumo wa mtandao wa ukusanyaji wa takwimu za kuwezesha kufanya tathmini sahihi umeharibika vibaya kutokana na ukosefu wa nyenzo na vitendea kazi. Jambo hili limesababisha udhaifu mkubwa kiutendaji na hivyo mipango mingi ya uendelezaji wa rasilimali za maji kutofanyiwa tathmini kamilifu. Jambo hili linaweza kusababisha usanifu dhaifu ambao unaweza kulitia hasara taifa kwa miradi kushindwa kukidhi matarajio, ama usanifu wa miradi ghali na hivyo taifa kutumia fedha nyingi.



Ili kuwa na msingi bora na endelevu wa kusimamia maendeleo na mipango ya matumizi ya rasilimali za maji:

- (i) Tathmini ya rasilimali za maji itafanywa kwa kutumia taarifa sahihi za kisayansi.
- (ii) Hali ya wingi na ubora wa maji yaliyopo juu na chini ya ardhi na matumizi yake, itaainishwa na kufanyiwa tathmini ya mara kwa mara kwa misingi ya kibonde na mikondo ya maji chini ya ardhi, na taarifa hizo kupatikana kiurahisi kwa watumiaji maji, wadau na wenye kutoa maamuzi.

4.4.2 Mipango na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

Lengo: Kuwa na mipango endelevu ya matumizi ya rasilimali za maji.

Miradi mingi ya kutumia rasilimali za maji imetekelezwa kissekta bila kuzingatia kikamilifu mahitaji ya sekta na wadau wengine. Matokeo yake ni kwamba miradi mingi ama haitimizi malengo yake, imekufa, au imekumbwa na uhaba wa maji wa mara kwa mara hadi kufikia hatua ya kujenga dhana ya kuanza kuhamisha maji kutoka Bonde moja na kuyapeleka kwenye Bonde lenye uhaba wa maji. Utekelezaji wa kuhamisha maji unaweza ukawa na madhara makubwa iwapo hapatakuwepo na taratibu, miongozo na vigezo vitakavyosimamia jambo hili. Aidha, uendeshaji wa miradi kama vile mabwawa ya uzalishaji umeme na miradi mikubwa ya umwagiliaji mashamba hauzingatii mahitaji ya mazingira na hivyo kuhatarisha uhai wa mifumo ya ikolojia na bayoanuai.

Mipango madhubuti ni mojawapo ya majukumu muhimu katika kusimamia rasilimali za maji. Masuala mbalimbali ya kiufundi na kisera yanajumuishwa katika kuendeleza na kusimamia mipango hii. Kwa muda mrefu uandaaji wa mipango ya rasilimali za maji umekuwa ukifanyika kissekta, kimkoa au kimradi hali ambayo imesababisha migongano miongoni mwa watumiaji wa maji.

Ili kuwa na mipango bora ya matumizi ya maji:

- (i) Mipango ya kutumia rasilimali za maji itafanywa kwa misingi ya Mabonde na kwa kushirikisha sekta na washikadau mbalimbali. Ngazi za mipango ya matumizi ya maji ni Taifa, Bonde, Wilaya na ngazi ya chini ya watumia maji. Aidha, mipango ya utekelezaji itajumuisha masuala ya matumizi ya ardhi, maji na mazingira.
- (ii) Uendelezaji wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi utafanywa kulingana na mipango ya Bonde husika.
- (iii) Miradi yote mikubwa ya maji ikiwa ni pamoja na ya ujenzi wa mabwawa makubwa, uvunaji wa maji ya mvua, milango ya kuchukua maji, vituo vya kusukuma maji na uchimbaji wa visima, matumizi ya maji chini ya ardhi na uhamishaji wa maji kutoka Bonde moja kwenda Bonde jingine; itatakiwa kufanyiwa tathmini kuhusu athari zake katika mazingira na kaputa kibali.

4.5 Takwimu na Taarifa

Lengo: Kuwa na takwimu na taarifa sahihi, zinazopatikana kwa wakati zinapohijiwa kwa ajili ya usanifu, ujenzi na uendeshaji wa miradi mbalimbali.

Takwimu na taarifa sahihi zinahitajika kuwezesha kufanya tathmini mbalimbali za hali ya maji, kuandaa mipango, ujenzi na uendeshaji wa miradi. Aidha, takwimu zinahitajika pia ili kuwezesha kufanya maamuzi na kuchukua hatua sahihi kuhusu shughuli za usimamizi, ugawaji na uendelezaji wa rasilimali za maji. Mfumo ulio bora wa usimamizi wa rasilimali za maji ni ule wenye uwezo wa kutoa takwimu na taarifa sahihi za wingi, ubora na matumizi ya maji kwa wakati unaotakiwa. Hivi sasa mtandao wa vituo vya ukusanyaji wa takwimu na



taarifa mbalimbali umevurugika kutokana na kukosekana kwa nyenzo na vitendea kazi na hivyo kuathiri mfumo mzima wa kupata taarifa na takwimu. Hali hii ya kukosekana kwa taarifa muhimu za maji kunafanya miradi isiwe endelevu, bali kuwa ya gharama kubwa kujenga, hafifu kiasi cha kutokuwa na ufanisi. Aidha, kukosekana kwa taarifa muhimu kunafanya mipango ya kukabiliana na majanga isiweze kuandaliwa na kutekelezwa kwa ukamilifu. Pamoja na udhaifu huo, kwa sasa hakuna mfumo madhubuti wa pamoja wa upatikanaji na usimamizi wa taarifa baina ya sekta zote husika na wadau mbalimbali.

Ili kuwa na taarifa sahihi za rasilimali za maji mambo yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Mfumo uliopo wa kukusanya, kuchambua, kuhifadhi takwimu na kutoa taarifa mbalimbali za rasilimali za maji utaimarishwa katika ngazi za Taifa na Mabonde. Aidha, uwezo wa kukusanya takwimu, kusimamia taarifa na kufanya tathmini ya rasilimali za maji utaimarishwa na utarahisishwa, wa gharama nafuu na unaozingatia mahitaji ya wadau.
- (ii) Uratibu na ubadilishanaji wa takwimu na taarifa miongoni mwa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi utaimarishwa ili kuongeza ujuzi, ufanisi na ushirikiano.
- (iii) Mamlaka za udhibiti katika ngazi ya Taifa na Bonde zitawezeshwa kisheria kupata takwimu mbalimbali kutoka kwa watumiaji wa maji.

4.6 Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia

Madhumuni: Kuboresha maarifa, taarifa na mawasiliano baina ya jamii na watumiaji maji.

Usimamizi wa rasilimali za maji unapaswa kujumuisha masuala ya mazingira, ikolojia na maendeleo ya jamii na uchumi kwa lengo la kutatua matatizo ya utoaji huduma. Hii ni pamoja na utafiti, kazi za kiufundi, udhibiti wa kiutawala na kisheria. Utafiti na uendelezaji wa mbinu za kisasa za kisayansi na kiteknolojia unahitajika ili kuleta ufanisi na kupunguza gharama. Hivi sasa shughuli za utafiti au uvumbuzi wa teknolojia nyepesi na ya gharama nafuu unafanywa kwa kiwango kidogo sana na sio endelevu. Aidha, hakuna uratibu baina ya sekta husika, na matokeo ya utafiti hayasambazwi kwa wadau. Kutokana na udhaifu huo, Taifa limeendelea kutumia teknolojia ambazo sio muafaka kwa mazingira ya nchi yetu.

Ili kuboresha shughuli za utafiti wa rasilimali za maji, yafuatayo yatafanyika:

- (i) Uanishaji wa mahitaji ya utafiti na maendeleo ya teknolojia utafanywa.
- (ii) Vituo vya utafiti na maendeleo ya teknolojia ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji vitaanzishwa, na juhudi za watafiti wa hapa nchini zitatambuliwa na kuhamasishwa.
- (iii) Ushirikiano kati ya taasisi za utafiti ndani na nje ya nchi utaimarishwa.

4.7 Mafunzo na Maendeleo ya Watumishi

Lengo: Kuwepo wataalamu wa kutosha wa kutekeleza kazi mbalimbali za rasilimali za maji.

Kazi zinazohusu rasilimali za maji ni pamoja na ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu, uanishaji na utumiaji wa takwimu, kufanya tathmini mbalimbali, ugawaji wa maji, ukaguzi na ufuatiliaji, uandaaji wa mipango ya matumizi ya maji, utafiti na kazi mbalimbali za kiutawala na utekelezaji wa sheria. Huduma hizi kwa ujumla zinahitaji utaalum na ujuzi maalum. Kwa sasa utekelezaji wa kazi hizi unaathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na ukosefu wa watumishi wa kutosha na mafunzo ya uendelezaji wa watumishi waliopo. Aidha, watumishi wa fani mbalimbali za rasilimali za maji wameendelea kupungua kutokana na kuacha kazi, kustaafu au vifo.



Kuwepo kwa utaalumu unaohitajika miongoni mwa watendaji, watumiaji na viongozi wa ngazi zote ni muhimu kwa ajili ya ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za maji. Kinachohitajika ni kuwepo kwa wataalam wenye ujuzi katika fani za haidrolojia, haidrojiolojia, ubora wa maji, sheria za maji, usuluhishi wa migogoro ya matumizi mbalimbali ya maji kitaifa, kutambua na kutumia teknolojia bora, pamoja na wataalamu wa mipango na usimamizi wa rasilimali za maji. Hivi sasa uwezo wa kushughulikia masuala mbalimbali yanayohusu rasilimali za maji unazidi kupungua kutokana na kutokuwepo wahitimu wa kutosha kutoka vyuo vyetu vya ufundi na vya elimu ya juu.

Ili kuwepo na wataalamu wa kutosha hatua zifuatazo zitachukuliwa:

- (i) Tathmini itafanywa kuhusu hali ya utumishi iliyoko hivi sasa ikilinganishwa na mahitaji na matokeo ya tathmini hiyo itakuwa ndiyo kigezo cha uandaaji wa mipango ya mafunzo kazini.
- (ii) Mipango ya kuajiri wataalamu mbalimbali katika fani ya usimamizi wa rasilimali za maji kulingana na mahitaji itaandaliwa na kutekelezwa.

4.8 Kujikinga na Majanga

4.8.1 Mafuriko

Lengo: Kuwa na mipango ya kujikinga na madhara ya mafuriko.

Katika nchi yetu majanga ya mafuriko yamekuwa yakitokea mara kwa mara. Kumeuwepo na mafuriko ya kawaida yanayotokana na mvua kubwa, na yale yanayotokana na maporomoko ya ardhi. Mafuriko katika Mabonde kama vile Rufiji yamesababisha vifo vya watu na upotevu wa mali na uharibifu wa miundombinu. Maafa ya mafuriko yamekuwa yakishughulikiwa bila ya kuwepo kwa taarifa kamili na pia uratibu wa kutosha baina ya sekta mbalimbali, na hivyo juhudi za kukabiliana nayo zimelewa zaidi katika kukabiliana na tukio la janga badala ya kujikinga ili kupunguza madhara. Aidha, hakuna miundombinu ya kihaidrolojia ya kutoa tahadhari ya juu ya uwezekano wa kutokea janga la mafuriko. Kutokana na udhaifu huo mafuriko makubwa yametokea kwa ghafla na hivyo kusababisha madhara makubwa.

Ili kuondoa udhaifu huu yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Vitaanzishwa vituo maalum vya kukusanya takwimu za mafuriko na kuimarisha vile vilivyopo vya kupima mitiririko ya maji, ili taarifa ziweze kupatikana mapema na wananchi kupata taarifa hizo mapema.
- (ii) Sehemu ambazo zipo hatarini kuathirika kwa mafuriko na maporomoko ya ardhi zitabainishwa na kuonyeshwa kwenye ramani.
- (iii) Wananchi watahamasishwa kutokujenga kwenye maeneo yenye uwezekano wa kukumbwa na mafuriko au maporomoko ya ardhi. Aidha, maeneo ya hatari yatatengwa na kuzuiwa kisheria.

4.8.2 Ukame

Lengo: Kupunguza madhara yatokanayo na ukame.

Ukame umekuwa ukitokea mara kwa mara na kusababisha kuharibika kwa mazao na hivyo kupunguza uhakika wa chakula, na kuathiri mifugo. Aidha, kupungua kwa wingi wa maji mitoni na kwenye mabwawa kumeathiri shughuli mbalimbali zinazotegemea maji kama vile uzalishaji umeme.

Ili kukabiliana na athari zitokanazo na ukame hatua zifuatazo zitachukuliwa:



- (i) Mipango ya kukabiliana na ukame itaandaliwa kwa kushirikiana na sekta na taasisi mbalimbali kama Wakala wa Hali ya Hewa.
- (ii) Utaratibu na vigezo vya kurekebisha migao ya maji uitaimarishwa ili kupunguza madhara ya ukame kwa sekta zote za huduma za jamii na uchumi.

4.8.3 Usalama na Umiliki wa Mabwawa

Lengo: Kuwa na taratibu za kuhakikisha usalama na umiliki wa mabwawa.

Mabwawa ni miundombinu muhimu ya kuinga maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuzuia mafuriko, kurekebisha mwenendo wa mito na kupunguza athari za mafuriko. Hata hivyo, ujenzi wa mabwawa kwenye mito unaambatana na kuhatarisha maisha na mali za watu wanaoishi ukanda wa chini ya mabwawa hayo kutokana na uwezekano wa mabwawa hayo kubomoka. Hivi sasa, hakuna miongozo imara na sheria inayoangalia suala zima la usalama, uandikishaji na umiliki, na ufuatiliaji wa mwenendo wa matumizi wa mabwawa. Mmomonyoko wa ardhi utokanao na matumizi ya ardhi na mvua husababisha mabwawa kujaa matope na hivyo kufupisha uhai wake, lakini hakuna kanuni zilizowekwa zinazohusu matumizi ya ardhi inayozunguka mabwawa kwa nia ya kuyalinda. Aidha, uendeshaji wa mabwawa usiozingatia kanuni na taratibu zilizowekwa unaweza pia kuhatarisha usalama wa mabwawa hayo na upotevu wa maji.

- (i) Mabwawa yatajengwa, kuendeshwa na kukarabatiwa na wamiliki kufuatana na miongozo na kanuni zitakazoandaliwa.
- (ii) Mabwawa yote yatamilikiwa na waliowekeza kwenye ujenzi wa mabwawa hayo kufuatana na miongozo na kanuni zitazoandaliwa.
- (iii) Maji yaliyomo kwenye mabwawa hayo yatamilikiwa na Serikali na taratibu za kuyatumia zitawekwa.
- (iv) Wamiliki wa mabwawa watatakiwa kuandaa mipango ya kuratibu na kufuatilia usalama wa mabwawa yao, na kuitekeleza kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa.

4.8.4 Majanga Yatokanayo na Uchafuzi wa Maji

Lengo: Kuweka utaratibu wa kujikinga na majanga yatokanayo na uchafuzi wa maji.

Majanga mengine yanatokana na uchafuzi wa ghafla wa maji juu au chini ya ardhi. Kwa mfano kupasuka kwa mabomba ya mafuta, kubomoka kwa viwanda vyenye kemikali za sumu na kupasuka kwa vyombo vya majini vyenye kemikali za sumu. Hali hii inaweza kusababisha uchafuzi mkubwa wa vyanzo vya maji, na hivyo kuathiri afya za binadamu, wanyama, viumbe hai na bayoanuai.

Ili kupunguza madhara yatokanayo na majanga haya, tathmini ya haraka ya mwenendo wa uchafuzi wa maji itafanyika na kutoa habari kwa vyombo husika. Usafirishaji wa bidhaa zenye sumu na za hatari utafuata kanuni na taratibu zilizopo.

4.9 Maji ya Kimataifa

Lengo: Kuwa na mfumo kamilifu wa kusimamia na kutumia maji ya kimataifa kwa misingi ya ushirikiano na haki.

Tanzania inashirikiana na nchi nyingine katika umiliki, utunzaji na matumizi ya rasilimali za maji ya kimataifa. Matumizi makubwa ya maji ya kimataifa kunahitaji maelewano na makubaliano baina ya nchi husika. Kimsingi mahitaji halisi ya matumizi ya maji ya kimataifa hayajaainishwa kwa Mabonde yote na pia mikakati kamilifu ya kuyatumia maji hayo haijaandaliwa kwa Mabonde yote. Rasilimali za maji ya kimataifa katika Mabonde yetu mbalimbali zina tabia na changamoto za kipekee katika usimamizi wake. Changamoto hizo ni



pamoja na (a) utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na masuala ya kuzuia uchafuzi wa maji, hifadhi ya bayoanuai na uharibifu wa maeneo oevu, uvuvi na udhibiti wa magugu maji. (b) uendelezaji wa mabonde ya maji na ujenzi wa miradi kama vile uzalishaji wa umeme, usambazaji wa maji ya kunywa na umwagiliaji, (c) urekebishaji na udhibiti kisheria wa mitiririko ya maji mitoni, na (d) uhamishaji wa maji kutoka Bonde moja kwenda Bonde jingine. Kwa ujumla mambo yote haya yanahitaji mikakati madhubuti ya usimamizi na uendelezaji wa maji ya Mabonde ya kimataifa.

Ili kuwa na mfumo kamilifu wa kusimamia kuendeleza na kutumia maji ya kimataifa, yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Itafanyika tathmini ili kubainisha kipaumbele cha Taifa katika utumiaji na uendelezaji wa rasilimali za maji katika Mabonde ya kimataifa kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya taifa.
- (ii) Maji ya Mabonde katika mito na maziwa tunayochangia kuyamiliki yatatumika kikamilifu kukidhi mahitaji kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi kwa kuzingatia misingi ya usawa, haki na uwiano mzuri. Aidha, tutakuza uwezo wetu wa kutumia rasilimali za maji ya kimataifa kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya taifa.
- (iii) Mfumo wa kusimamia na kutumia rasilimali za maji katika Mabonde ya kimataifa utaandaliwa na kutekelezwa kwa msingi wa kukuza ushirikiano. Aidha, ushirikiano wa kiufundi, na hasa kwenye nyanja za utafiti, ukusanyaji wa takwimu na kupeana taarifa, utapewa msukumo.

4.10 Mfumo wa Kitaasisi

Lengo: Kuwa na mfumo imara wa kusimamia rasilimali za maji.

Usimamizi wa rasilimali za maji unahitaji mfumo wa kitaasisi wenye uwezo wa kutekeleza majukumu makuu ya (i) utafutaji wa maji, (ii) kutathmini wingi na ubora wa maji, (iii) kugawa maji, (iv) kudhibiti uchafuzi wa maji, na (v) shughuli zenye mwingiliano kisekta katika utunzaji wa mazingira, uandaaji wa mipango na uendelezaji wa Ofisi za Mabonde. Aidha, vyombo imara vya kiutawala na kitaasisi ndivyo vitakavyokuwa na jukumu la kusimamia na kutekeleza Sheria ya Maji.

Ili kuwa na mfumo madhubuti wa usimamizi wa rasilimali za maji:

- (i) Mfumo wa kitaasisi uliopo utafanyiwa mapitio na kurekebishwa ili kuweza kukabiliana na changamoto ya usimamizi wa rasilimali za maji na kuandaa mipango inayohitajika. Wajibu na majukumu ya wadau mbalimbali yatafafanuliwa katika mfumo huo mpya, na kuhakikisha kuwa wawakilishihalali wa wadau wanashikiri.
- (ii) Muundo na taratibu za kiutawala vitatayarishwa ili kuwezesha ushirikishwaji wa mamlaka zenye majukumu katika ngazi mbalimbali na kuongeza uwezo wa mabonde kujitegemea. Aidha, mfumo wa kukusania na kutoa taarifa, ulio sahihi, wenye uwazi na unaozingatia uwajibikaji utawekwa.

Uratibu na Ushirikiano

Usimamizi wa rasilimali za maji ni shughuli inayohusisha sekta mbalimbali na inahitaji mfumo mzuri wa uratibu na ushirikiano katika ngazi zote. Mifumo ya uratibu na ushirikiano inayorahisisha ubadilishanaji taarifa ili kuwezesha wadau kuelewa matatizo, mafanikio na mahitaji, na ambayo inasaidia pia kubadilishana mawazo juu ya uzoefu na ufumbuzi wa matatizo mbalimbali na mbinu za utekelezaji kwa pamoja zitaanzishwa na kuimarishwa.



Vyombo vya Kiutekelezaji na Utatuzi wa Migongano

Tanzania imegawanywa katika mabonde tisa. Mipaka ya Mabonde ya mito katika nchi yetu hailingani na mipaka ya kiutawala kama vile Mkoa na Wilaya. Kwa kuzingatia umuhimu huo kutakuwa na ngazi kuu tano; Ngazi ya Kitaifa, Ngazi ya Bonde, Ngazi ya Bonde Dogo, Ngazi ya Wilaya na Ngazi ya Mwanzo ambayo ni ngazi ya watumia maji ambayo itahusu vyama vya watumia maji ambavyo vitawaunganisha watumiaji wa chanzo kimoja.

Ngazi ya Taifa

Wizara inayohusika na maji ndiyo msimamizi mkuu wa rasilimali za maji nchini. Itakuwa na majukumu ya kuandaa Sera na Sheria, kuandaa mazingira mazuri na kushirikisha sekta mbalimbali, kuainisha mahitaji ya maji ya sekta nyingine na kuandaa na kusimamia mipango ya matumizi ya maji, kufanya tathmini ya maji, kukusanya taarifa mbalimbali za maji na kutoa taarifa mbalimbali, kuandaa na kutunza benki ya takwimu za rasilimali za maji, kuandaa na kutoa mafunzo. Wizara inayohusika na maji itaandaa kanuni mbalimbali za kisheria, na Waziri kusikiliza rufaa mbalimbali na kuzitolea uamuzi. Aidha, katika ngazi ya taifa, Bodi Kuu ya Maji iliyopo itafanyiwa marekebisho na kupewa majukumu mapya ya uandaaji wa mipango ya kisekta kwa pamoja kuhusu usimamizi na matumizi ya Rasilimali za Maji nchini na kutatua migogoro ihusuyo maji kitaifa kama vile migogoro baina ya sekta mbalimbali. Pia, Wizara husika itasimamia Sheria ya Maji, kuandaa mipango ya matumizi ya maji na kuratibu mipango ya maji katika Mabonde.

Ngazi ya Mabonde

Kwa vile usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji utafanywa kimabonde, ngazi hii ndio mahala pa shughuli zote za ukusanyaji na uainishaji wa takwimu, ugawaji wa maji, uzuiaji wa uchafuzi wa rasilimali za maji, uandaaji wa mipango ya matumizi ya maji, ukusanyaji wa ada na mapato mbalimbali na utatuzi wa migongano inayohusu matumizi ya maji. Utaratibu wa sasa wa kuwa na Bodi za Maji za Mabonde na Ofisi za Maji za Mabonde utaimarishwa.

Ngazi ya Mabonde Madogo

Ukubwa wa Mabonde yetu ya Mito unaifanya kazi ya usimamizi kuwa ngumu na watendaji kuwa mbali na watumia maji. Ili kuondokana na tatizo hili Bodi ama Kamati za Mabonde madogo zitaanzishwa. Ngazi hii itaundwa na wawakilishi kutoka mashirika, taasisi na vyama vya watumia maji yaliyomo kwenye Bonde husika. Majukumu ya Bodi za Mabonde madogo ni kusimamia kwa karibu utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya maji na utatuzi wa migogoro kama ilivyo kwa ngazi ya Bonde.

Ngazi ya Wilaya

Halmashauri za Wilaya na Serikali za Mitaa zitashiriki kikamilifu katika Bodi za Mabonde na za Mabonde Madogo. Zitawajibika katika kupanga na kuendeleza miradi ya maji kulingana na mipango ya Bonde kwa ujumla, kutoa ushauri wa kitaalam kwa watumiaji wa maji katika Wilaya zao, kulinda na kuhifadhi maliasili katika maeneo ya Vijiji na Kata, kuunda Sheria ndogondogo za usimamizi wa rasilimali za maji, na utatuzi wa migogoro kulingana na Sheria na kanuni zilizopo. Aidha, Halmashauri za Wilaya zitaainisha mahitaji ya maji kwa maendeleo ya Wilaya na kushiriki katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya maji ya Bonde.

Ngazi ya Mwanzo ya Watumiaji Maji

Vyama au umoja wa watumiaji maji ndio itakuwa ngazi ya mwanzo ya kusimamia rasilimali za maji. Vyama hivi vitakuwa na majukumu ya kusimamia matumizi ya maji waliyogawiwa,



kutatua migogoro ya maeneo yao, kukusanya taarifa na takwimu mbalimbali, kushiriki katika kuandaa mipango mbalimbali ya kutumia maji. Vyama hivi ndivyo vitakavyounda Kamati za Maji za Mito, na vitatoa wawakilishi kwenye Bodi za Mabonde Madogo. Watumiaji maji wanao wajibu wa kutunza mazingira ya maeneo yao ya vyanzo vya maji, kutumia maji kwa uangalifu na ufanisi, kuhakikisha kuwa maji wasioyahitaji yanarudishwa mtoni, kutekeleza matakwa ya Sheria na maelekezo yaliyomo kwenye hati zao za maji, na kuzuia uchafuzi wa maji. Ngazi hii itakuwa na wawakilishi halali katika Bodi za Maji na Kamati za Mabonde Madogo.

Ushirikishaji Jamii

Jamii kwa ujumla inalo jukumu kubwa katika sekta ya maji, kwani ndiyo mlinzi na msimamizi wa vyanzo vya maji. Katika ngazi zote za usimamizi wa maji ushiriki wa wanaume na wanawake kwenye maamuzi, mipango, usimamizi na utekelezaji wa rasilimali za maji utaimarishwa. Vijana na watoto kama wasimamizi wa rasilimali za maji kwa siku zijazo, watafundishwa kuhusu usimamizi, utunzaji, hifadhi na uendelezaji wa rasilimali za maji, kwani wao ndio wawezeshaji wa mabadiliko. Hii itawawezesha kuwa wasimamizi wazuri kwa siku zijazo.

4.11 Mfumo wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji

Lengo: Kuwa na mfumo madhubuti wa kisheria wa usimamizi wa rasilimali za maji.

Sheria ya Matumizi ya Maji ya 1974 na marekebisho yake ndiyo Sheria mama inayosimamia matumizi ya rasilimali za maji na uzuiaji wa uchafuzi wa vyanzo vya maji. Hata hivyo Sheria hii haikidhi mahitaji halisi ya sasa. Sheria hii inahitaji kufanyiwa mapitio ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika kusimamia rasilimali za maji. Mapitio na marekebisho hayo pia yatahusu uainishaji wa Sheria ya Matumizi ya Maji na Sheria nyingine zinazohusiana.

Ili kuwa na mfumo madhubuti wa kisheria wa usimamizi wa rasilimali za maji yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Sheria ya matumizi na udhibiti wa maji pamoja na sheria ndogo ndogo na kanuni mbalimbali zitafanyiwa mapitio na ulinganifu ili kukidhi mahitaji ya sasa. Katika marekebisho hayo vyombo vya kusimamia rasilimali za maji vitapewa majukumu zaidi ili kuviwezesha: (a) kusimamia Sheria, kanuni na taratibu za kugawa, kutumia maji na kudhibiti uchafuzi, (b) kuwa na mamlaka ya kukusanya mapato kutokana na malipo mbalimbali yatokanayo na huduma za rasilimali za maji, (c) kuwezesha kuundwa kwa vyombo mbalimbali vingine vya ngazi za chini ya Bonde ambavyo vitatambuliwa kisheria kwa lengo la kuwaunganisha watumia maji na wadau wengine na vinavyowakilisha watumiaji maji wa chanzo kimoja, na (d) kuwa vitovu vya kusuluhisha migongano inayohusu ugawaji, utumiaji, na uchafuzi wa maji.
- (ii) Sheria za kimila zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji zitakazoonekana kufaa zitaainishwa na ile Sheria ya Matumizi ya Maji.

4.12 Kugharamia Usimamizi wa Rasilimali za Maji

Lengo: Kuwa na mfumo endelevu wa upatikanaji fedha kwa ajili ya kugharamia usimamizi wa rasilimali za maji.

Usimamizi wa rasilimali za maji unajumuisha masuala ya kiufundi, kiutawala na kisheria ambayo utekelezaji wake unahitaji fedha. Masuala haya ni pamoja na utafiti, uratibu, ugawaji wa maji, udhibiti wa uchafuzi, ufuatiliaji, kusimamia sheria, utunzaji wa mazingira, na kuandaa mipango na uendelezaji wa Mabonde ya maji. Uhaba wa fedha umechangia kuwa na miundombinu hafifu ya kukusanyia takwimu muhimu za shughuli hizo. Ili kuweza kufanikisha malengo ya usimamizi bora wa rasilimali za maji:



Matumizi yote ya maji hususan ya shughuli za kiuchumi, yatatozwa ada. Aidha, aina na viwango vya ada na vigezo vitakavyotumika vitafanyiwa mapitio ya mara kwa mara kulingana na matokeo ya tafiti zitakazofanywa.



SEHEMU II: HUDUMA YA MAJI VIJIJINI

1. MAELEZO YA JUMLA



Inakadiriwa kuwa 80% ya wakazi wapatao milioni 34 nchini wanaishi vijijini. Pamoja na jitahada kubwa za kuwekeza kwenye huduma ya maji vijijini tangu mwanzoni mwa miaka ya 1970, kwa sasa ni 50% tu ya wakazi wa vijijini ndio wanaopata huduma ya maji. Hata hivyo, kutokana na matatizo mbalimbali ya usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji, zaidi ya 30% ya miradi hiyo haifanyi kazi vizuri.

Tathmini ya sekta ya maji iliyofanyika mwaka 1995 ilibainisha mapungufu mbalimbali katika Sera ya Maji ya 1991. Miongoni mwa mapungufu hayo ni pamoja na kutoipa umuhimu Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma ya maji, kutokushirikisha kikamilifu wadau mbalimbali hususan wananchi na mapungufu katika mifumo ya kitaasisi na kisheria. Matokeo ya tathmini hiyo yalilazimu kuifanyia mapitio Sera ya Maji ya 1991, ikiwa ni pamoja na mambo yanayohusu huduma ya maji vijijini. Lengo lilikuwa ni kuainisha mikakati itakayotumika katika utekelezaji wa Sera hii ili kufikia madhumuni ya Sera kwa maeneo ya vijijini. Sehemu hii ya Sera imeandaliwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali katika hatua tofauti.

2. MADHUMUNI

Madhumuni ya jumla ya sera kuhusu utoaji wa huduma ya maji vijijini ni kuboresha afya ya jamii na kusaidia kuondoa umaskini vijijini kwa kuboresha upatikanaji wa maji safi, salama na ya kutosha.

Madhumuni mahsusi ni kama yafuatavyo:

- (i) Upatikanaji wa huduma endelevu ya maji safi, salama na ya kutosha, kwa gharama iliyo ndani ya uwezo wa wananchi vijijini.
- (ii) Kuweka bayana majukumu na wajibu wa wadau mbalimbali.
- (iii) Kuweka mkazo kuhusu wananchi kulipia sehemu ya gharama za ujenzi wa miradi, na pia kulipia gharama zote za uendeshaji na matengenezo ya miradi yao, tofauti na dhana iliyokuwepo ya kuchangia tu sehemu ya gharama za uendeshaji na matengenezo.
- (iv) Kubadili utaratibu wa huduma ya maji, kutoka kwenye ule uliozoeleka wa kuletewa huduma, kwenda kwenye ule wa wananchi kubuni, kuanzisha na kuendesha miradi yao wenyewe.
- (v) Uendeshaji na matengenezo ya miradi kuwa katika ngazi ya chini kadiri iwezekanavyo, tofauti na utaratibu uliozoeleka wa matengenezo kufanywa na ngazi za juu.
- (vi) Kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika kugharamia, kujenga, kuendesha na kutoa huduma ya maji vijijini.
- (vii) Kuboresha afya ya jamii kwa kuunganisha mipango ya utoaji wa huduma ya maji, usafi wa mazingira na elimu ya afya.

3. MISINGI

Uandaaji wa Sera kuhusu huduma ya maji vijijini umeongozwa na misingi mikuu minne ambayo imetokana na uzoefu uliopatikana katika kutekeleza Sera ya Maji ya 1991, pamoja na uzoefu kutoka nchi nyingine zinazoendelea. Misingi hiyo ni ya Kijamii, Kiuchumi, Mazingira na ya Uendelevu.



3.1 Misingi ya Kijamii

Maji ni Hitaji la Msingi na Haki ya Kila Mtu

Kwa kutambua kuwa upatikanaji wa maji safi na salama ni hitaji la msingi na haki ya kila mtu, utoaji wa huduma ya maji vijijini utaimarishwa.

Matumizi ya Maji kwa ajili ya Binadamu Kupewa Umuhimu wa Kwanza

Katika utoaji wa huduma ya maji vijijini, matumizi ya maji kwa ajili ya binadamu yatapelelewa umuhimu wa kwanza.

Maeneo Yenye Uhaba wa Maji Kupewa Kipaumbele Kwenye Ujenzi wa Miradi

Sehemu nyingi za nchi ni kame na zina upungufu mkubwa wa maji. Kipaumbele kitawekwa kwenye upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo katika maeneo yenye uhaba wa maji.

3.2 Misingi ya Kiuchumi

Maji ni Bidhaa ya Kiuchumi

Kwa kutambua umuhimu wa mchango wa maji katika uzalishaji mali kwa upande mmoja, na kwa kuzingatia kwamba kiasi kikubwa cha fedha kinahitajika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji kwa upande mwingine, upatikanaji wa huduma ya maji kwa ajili ya shughuli za uzalishaji utachukuliwa kama suala la kiuchumi, linalohitaji kusimamiwa kwa ufanisi na kugharimiwa na watumiaji.

3.3 Misingi ya Mazingira

Kulinda na Kuhifadhi Vyanzo vya Maji

Ili kutoa huduma endelevu maeneo ya vyanzo vya maji kwa ajili ya miradi ya maji vijijini yataipimwa na watumiaji watahamasishwa kuomba hati miliki ya ardhi kupitia vyombo vyao vya usimamizi.

Uimarishaji wa Hifadhi ya Mazingira

Wakati wa kubuni na kupanga miradi ya maji, tathmini ya athari za mazingira itafanyika na hatua za kuthibiti athari hizo zitaainishwa na kuzingatiwa wakati wa ujenzi na uendeshaji wa miradi husika.

Kuboresha Afya ya Jamii kwa Kuzingatia Usafi wa Mazingira na Elimu ya Afya

Afya ya jamii italindwa kwa kuhamasisha wananchi juu ya matumizi bora ya vyoo, kutotupa takataka ovyo na umuhimu wa upatikanaji wa huduma ya maji ya kutosha na salama.

3.4 Misingi ya Huduma Endelevu

Ujenzi na uendeshaji endelevu wa miradi ya maji vijijini, utategemea kubainisha waziwazi majukumu na wajibu wa watendaji mbalimbali, pamoja na makundi mbalimbali ya wadau. Ili kuhakikisha kuwa ujenzi na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini unakuwa endelevu, mambo yafuatayo yatazingatiwa:



- (i) Uendeshaji na matengenezo ya miradi kufanyika kwenye ngazi ya chini karibu na walengwa kadiri inavyowezekana.
- (ii) Walengwa wenyewe kubuni, kumiliki, kusimamia na kuiendesha miradi yao ya maji.
- (iii) Kuhakikisha kuwa gharama za uendeshaji, matengenezo, ukarabati na upanuzi wa miradi zinalipwa na wanaotumia huduma hiyo.
- (iv) Kuhakikisha kuwa vipuli na utaalum wa kiufundi vinapatikana ili matengenezo na ukarabati wa miradi ya maji ufanyike bila kuchelewa, kwa kuchagua na kutumia viwango na aina chache ya vifaa na mitambo inayostahili kutumika, na pia kwa kushirikisha Sekta Binafsi.
- (v) Kulinda vyanzo vya maji na maeneo yanayozunguka vyanzo hivyo.
- (vi) Kuhakikisha kuwa kuna uwiano mzuri kati ya teknolojia iliyochaguliwa na kiwango cha huduma na upatikanaji wa maji kwa upande mmoja, na uwezo wa kiuchumi wa watumiaji maji wenyewe kwa upande mwingine.
- (vii) Kutambua kuwa wanawake ni miongoni mwa wahusika wakuu katika utoaji wa huduma ya maji vijijini.

4. MASUALA YA SERA KUHUSU HUDUMA YA MAJI VIJIJINI

Kufanikiwa kwa Sera kutahitaji mikakati mbalimbali inayokwenda na wakati, ili iende sambamba na mabadiliko ya hali na mahitaji halisi yanayojitokeza. Kwa kuzingatia misingi ya Sera yenyewe, madhumuni ya Sera yanatarajiwa kufikiwa kwa kuangalia masuala yafuatayo:

4.1 Ushirikishaji wa Jamii

Kumiliki miradi ya maji vijijini

Lengo: Kuwa na miradi ya maji endelevu inayomilikiwa na jamii kisheria.

Miradi iliyojewa bila kushirikisha walengwa katika kuibuni, kuipanga na kuisimamia, mara nyingi haipati matengenezo kama inayostahili, na hivyo kuifanya isiwe endelevu. Watumiaji wa huduma itolewayo na miradi kama hiyo, hawaioni kama ni yao na wala watumiaji hao hawamilikishwi miradi hiyo kisheria. Hali hii hufanya watumiaji waone kuwa hawahusiki na uendeshaji na matengenezo ya miradi hiyo. Ili kutatua tatizo hili, jamii zitahamasishwa na kuwezesha katika kubuni, kumiliki kisheria na kusimamia miradi yao ya maji, ikiwa ni pamoja na visima vya maji.

Ili kuwa na miradi endelevu inayomilikiwa na jamii kisheria, yafuatayo yatafanywa:

- (i) Utaandaliwa utaratibu wa kusajili vyombo vya watumiaji maji kisheria, ili kuhakikisha kuwa wananchi ndio wamiliki wa miradi yao ya maji, ikiwa ni pamoja na visima vya maji.
- (ii) Majukumu, wajibu, haki, mipaka na mamlaka ya vyombo vya watumiaji maji yatawekwa bayana.
- (iii) Wananchi watawezesha kupata ujuzi wa kiufundi na wa kusimamia miradi ya maji.

Kuchagua teknolojia inayofaa

Lengo: Kuhakikisha kwamba wananchi wanachagua teknolojia inayowafaa.

Kuharibika kwa miradi ya maji vijijini kunasababishwa na mambo mbalimbali, yakiwemo ya uchaguzi wa teknolojia isiyofaa, kujenga miradi katika maeneo yasiyostahili, walengwa kutokubali kupokea mradi kutokana na sababu za kijamii, na watumiaji kutokuwa na uwezo wa kumudu gharama za ujenzi na uendeshaji wa miradi hiyo.

Ili kuwa na uchaguzi wa teknolojia inayofaa:



- (i) Wananchi watapewa uwezo na mamlaka ya kuchagua teknolojia inayowafaa kwa kuzingatia kiwango cha huduma wanayoweza kuimudu, hususan ambayo gharama zake za ujenzi, uendeshaji na matengenezo ni nafuu kwao.
- (ii) Matumizi ya teknolojia ambazo hazichafui mazingira kama vile maji ya mtiririko, teknolojia inayotumia mionzi ya jua au upepo kwa kusukuma maji yatahimizwa, na jamii itahamasishwa kutumia teknolojia hizo.

Kushirikisha wananchi katika kubuni, usanifu na ujenzi wa miradi

Lengo: Kuwa na watumiaji maji wanaotambua kuwa miradi ya maji ni yao.

Wananchi wanahitaji wahamasishwe ili waweze kushiriki kikamilifu katika kubuni, kupanga kusanifu, kujenga na kusimamia miradi yao ya maji, na hivyo kujenga uwezo wao wa kutambua kuwa wao ni wamiliki wa miradi, na pia hatua kwa hatua kujenga uwezo wao wa kusimamia usanifu, ujenzi na uendeshaji wa miradi yao. Aidha, wananchi watawezesha na watawajibika katika kuwekeana mikataba na wataalamu washauri na makandarasi mbalimbali kuhusiana na usanifu na ujenzi wa miradi ya maji. Wananchi wanaweza kuomba msaada kutoka halmashauri za wilaya, tawala za mikoa na taasisi nyingine kwa ajili ya kuandaa na kusimamia mikataba hiyo.

Ili kuhakikisha kuwa wananchi wanashiriki kikamilifu katika kubuni, kupanga, usanifu, ujenzi na usimamizi wa miradi yao yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Miongozo ya kusanifu miradi itafanyiwa mapitio na kusambazwa.
- (ii) Wananchi watapewa mafunzo ili kupata ujuzi wa kuwekeana na kusimamia mikataba inayohusu usanifu na ujenzi wa miradi ya maji.

Kushirikisha wananchi katika uendeshaji na matengenezo ya miradi

Lengo: Kuwa na mfumo endelevu wa uendeshaji na matengenezo ya miradi.

Miradi itakuwa endelevu endapo wananchi watawajibika kulipa gharama zote za uendeshaji na matengenezo, na zile za uboreshaji wa huduma ili kuinua kiwango na ubora wa upatikanaji wa huduma ya maji. Aidha, wananchi watawajibika kusimamia uendeshaji na matengenezo ya miradi yao. Katika kubuni miradi, gharama za uendeshaji na matengenezo zitajadiliwa kwa pamoja na walengwa ili kulinganisha kiwango cha ubora wa huduma inayotakiwa, teknolojia itakayochaguliwa, utashi na uwezo wa wananchi katika kuendesha, kutengeneza na kuisimamia miradi hiyo. Wananchi wanaweza kuingia mikataba na waendeshaji binafsi kuhusu uendeshaji na matengenezo ya miradi yao.

Ili kuhakikisha kuwa miradi inakuwa endelevu, yafuatayo yatafanywa:

- (i) Wananchi watahamasishwa na kuwezesha ili wawajibike kusimamia na kulipa gharama zote za uendeshaji na matengenezo, na zile za uboreshaji wa huduma.
- (ii) Wananchi watapewa mafunzo ya kuwawezesha kuingia na kusimamia mikataba na waendeshaji binafsi.

4.2 Kushirikisha Sekta Binafsi katika Kutoa Huduma ya Maji Vijijini

Lengo: Kuongeza kasi ya kupanua huduma ya maji vijijini ambayo ni endelevu.

Kwa muda mrefu, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijini vimekuwa vikifanywa na Sekta ya Umma. Sekta Binafsi ni changa, na inashirikishwa kwa nadra katika



utoaji wa huduma ya maji vijijini na hivyo kuchangia katika kudumaa kwake. Ushirikishaji wa Sekta Binafsi ni muhimu katika kuongeza kasi ya kupeleka huduma ya maji vijijini.

Ili kuhakikisha kuwa Sekta Binafsi inashiriki kikamilifu, hatua zifuatazo zitachukuliwa:

- (i) Sekta Binafsi itahamasishwa kuhusu nafasi za uwekezaji katika utoaji wa huduma ya maji vijijini.
- (ii) Mazingira mazuri, ikiwa ni pamoja na kuweka vivutio na kutambuliwa kisheria, yatawekwa ili kuiwezesha Sekta Binafsi kushiriki kikamilifu.
- (iii) Msaada utatolewa kwa Sekta Binafsi pamoja na Halmashauri za Wilaya ili kuinua uwezo wa kutoa huduma ya maji vijijini.
- (iv) Wananchi wataelimishwa kuhusu umuhimu wa kushirikisha Sekta Binafsi.

4.3 Jukumu la Sekta ya Umma katika Udhhibiti, Uwezeshaji na Uratibu wa Sekta ya Maji Vijijini

Lengo: Kuongeza tija.

Hadi hivi karibuni, Serikali Kuu imekuwa ndiyo mtekelezaji mkuu wa mipango ya maji. Ili kwenda sambamba na mabadiliko yanayoendelea katika sekta ya umma, mkakati ni Serikali kuwa mdhibiti, mwezeshaji na mratibu badala ya kuwa mtekelezaji.

Ili kutekeleza majukumu haya, yafuatayo yatafanywa:

- (i) Mfumo bora wa kisheria, unaosimamia utoaji huduma ya maji vijijini utawekwa.
- (ii) Misaada ya kiufundi na kifedha, kwa ajili ya ujenzi wa miradi mipya, upanuzi na ukarabati wa miradi iliyopo, itatolewa.
- (iii) Wizara inayohusika na maji pamoja na Halmashauri za Wilaya zitaimarishwa ili ziweze kutekeleza majukumu yake mapya ipasavyo.

4.4 Kiwango cha Chini cha Utoaji Huduma ya Maji Vijijini

Lengo: Kuweka kiwango cha chini cha utoaji huduma ya maji vijijini.

Matumizi halisi ya maji vijijini ni kati ya lita 5 kwa mtu kwa siku katika maeneo yenye uhaba mkubwa wa maji, na lita 30 kwa mtu kwa siku kwa maeneo mengine. Kwa ujumla, maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, ambayo mara nyingi siyo salama, hupatikana mbali na makazi ya watu.

Katika kutoa huduma ya maji vijijini, kiwango cha chini cha maji kwa matumizi ya nyumbani katika vipindi vyote vya mwaka, kitakuwa lita 25 za maji safi na salama kwa mtu kwa siku. Kiasi hicho cha maji kitapatikana kwenye vituo vya kuchotea maji vilivyoko kwenye umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye makazi ya watu, na kila kituo kitahudumia watu 250. Viwango vya juu zaidi kama vile uunganishaji wa maji majumbani au kituo kimoja kuhudumia chini ya watu 250, vitakubalika na kuhimizwa pale ambapo tathmini ya kiufundi inaruhusu, na pia kuzingatia matakwa na uwezo wa kufanya hivyo.

4.5 Maji kwa Ajili ya Mifugo

Lengo: Kuwa na maji ya kutosha kwa ajili ya mifugo.

Zaidi ya 90% ya mifugo ipo vijijini, na wananchi walio wengi katika mikoa kame ni wafugaji. Sehemu kubwa ya maeneo muhimu ya ufugaji ina uhaba mkubwa wa maji. Mara nyingi mahitaji ya maji kwa ajili ya mifugo hayajumuishwi kwenye usanifu wa miradi ya maji vijijini.



Ukosefu wa maji kwa ajili ya mifugo husababisha wafugaji kuhamahama wakitafuta maji na hivyo kusababisha uharibifu wa vyanzo vya maji na migogoro ya matumizi ya maji.

Ili kuhakikisha kuwa mifugo inapatiwa huduma ya maji ya kutosha, serikali itafanya yafuatayo:

- (i) Mkazo utawekwa kwenye ujenzi wa mabwawa, malambo na visima vya maji kwa ajili ya mifugo.
- (ii) Kujumuisha mahitaji ya maji kwa ajili ya mifugo kwenye usanifu wa miradi ya maji.
- (iii) Maeneo ya mifugo yenye uhaba wa maji yataainishwa na kupewa kipaumbele katika utoaji wa huduma ya maji kulingana na umuhimu wake.

4.6 Uvunaji wa Maji ya Mvua

Lengo: Kuongeza Upatikanaji wa Maji Vijijini kwa Kuvuna Maji ya Mvua.

Uvunaji wa maji ya mvua ni njia muhimu ya kupata maji hususan katika maeneo kame, ambako yanaweza kuwa ndio chanzo pekee cha maji cha kuaminika katika kipindi cha kiangazi.

Ili kuongeza matumizi ya teknolojia ya uvunaji maji ya mvua hatua zifuatazo zitachukuliwa:

- (i) Wananchi waishio vijijini watahamasishwa kutumia teknolojia hii.
- (ii) Utafiti kuhusu teknolojia za kuvuna maji ya mvua utaendelezwa.
- (iii) Uvunaji wa maji ya mvua utaimarishwa kwa kutoa elimu na mafunzo kwa wadau mbalimbali.

4.7 Kuunganisha Huduma za Maji, Usafi wa Mazingira na Elimu ya Afya

Lengo: Kuunganisha Huduma za Maji, Usafi wa Mazingira na Elimu ya Afya ili kuwa na jamii yenye afya bora vijijini.

Ukosefu wa maji safi na salama, na kutofuata kanuni za afya na usafi wa mazingira, ni vyanzo vikubwa vya magonjwa na vifo vya watu nchini. Aidha, hali hiyo ni sababu mojawapo ya umaskini, na hasa kwa wanawake na watoto, kwani wao ndio huathirika zaidi kutokana na mazingira duni ya kuishi, magonjwa na kutokuwa na fursa sawa ndani ya jamii. Utoaji wa elimu ya afya huanua kiwango cha afya inayotokana na huduma za maji na usafi wa mazingira, ikilinganishwa na utoaji wa huduma ya maji pekee bila elimu ya afya.

Ili kuboresha afya ya jamii, mkazo utawekwa kwenye mipango ya pamoja inayojumuisha utoaji wa huduma za maji, usafi wa mazingira na elimu ya afya.

4.8 Mwamko wa Kijinsia

Lengo: Jinsia zote kushiriki kikamilifu katika miradi ya maji.

Ingawa wanawake ndio watafutaji wa maji na watunzaji wa mazingira ya nyumbani, mfumo wa kitaasisi wa kuendeleza na kusimamia miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini hauzingatii hilo. Juhudi za makusudi zitafanywa ili kuhamasisha, kutoa mafunzo na kuwezesha wanawake pamoja na wanaume kushiriki kikamilifu kwenye miradi ya maji katika hatua zake zote.

Ili kuhakikisha kunakuwepo mwamko wa kijinsia, yafuatayo yatafanyika:

- (i) Uwakilishi wa jinsia zote kwenye vyombo vya watumiaji maji vijijini utahimizwa.



- (ii) Ushirikishwaji wa wanawake na wanaume katika kutoa maamuzi, utekelezaji na tathmini ya miradi ya maji utahimizwa.
- (iii) Mipango ya maji vijijini itazingatia mahitaji na vipaumbele vya wanawake na wanaume kwa kuzingatia uwezo wao wa kusimamia, kuendesha na kulipia.

4.9 Udhhibiti wa Utoaji Huduma ya Maji Vijijini

Lengo: Kuwa na huduma endelevu inayokidhi mahitaji ya makundi mbalimbali ya watumiaji maji.

Kwa kuzingatia kuwa huduma ya maji ni hitaji la msingi na haki ya kila mtu, ni muhimu maji kutumika kwa uangalifu na kwa uwiano mzuri kwa watu wote ndani ya jamii, hii ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma hii kwa makundi mbalimbali yasiyokuwa na uwezo kama vile maskini, wazee na walemavu. Halmashauri za Wilaya na zile za Vijiji zitadhibiti utoaji wa huduma utakaofanywa na vyombo mbalimbali vya watumiaji maji vijijini. Wananchi watahakikisha kuwa wanalinda na kuhifadhi vyanzo vyao vya maji, pamoja na kudhibiti utoaji wa huduma ya maji kwa uwiano mzuri kwa makundi mbalimbali ya jamii yasiyokuwa na uwezo wa kulipia huduma hiyo.

Ili kufanikisha shughuli hii, yafuatayo yatafanywa:

- (i) Majukumu, wajibu, haki na mipaka ya mamlaka ya vyombo vya watumiaji maji, yatawekwa bayana.
- (ii) Wananchi wataelimishwa kuhusu umuhimu wa kutunza, kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji.
- (iii) Taratibu zitawekwa za kuhakikisha kuwa vyombo vya watumiaji maji vinawajibika kwa watumiaji maji kwa kutoa huduma bora ya maji na watumiaji maji nao wanatekeleza wajibu wao, ikiwa ni pamoja na kulipia ankara zao za maji.

4.10 Kugharamia Miradi ya Maji Vijijini

Lengo: Wananchi washiriki kugharamia miradi yao ya maji vijijini.

Kupatikana kwa fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa miradi ni jambo la msingi katika kufanya miradi ya maji vijijini kuwa endelevu. Kutegemea Serikali na wahisani kama ndio pekee wenye jukumu la kugharamia utoaji wa huduma kumesababisha utoaji wa huduma ya maji vijijini kutofikia kiwango cha kuridhisha. Jamii itahamasishwa na kuwezesha ili iwe mstari wa mbele katika juhudi mbalimbali za kujenga na kuendesha miradi yao ya maji. Aidha, kwa kuzingatia kuwa maji ni hitaji la msingi na haki ya kila mtu na kwamba wananchi wengi bado hawana uwezo wa kulipia gharama za ujenzi wa miradi, Serikali Kuu na Halmashauri za Wilaya zitaendelea kusaidia wananchi katika ujenzi wa miradi yao ya maji. Kabla ya kupata msaada wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji, jamii husika itatakiwa kuthibitisha uwezo wake wa kuiendesha na kuifanyia matengenezo. Aidha, Jamii itatakiwa kulipia kwa fedha taslim sehemu ya gharama za ujenzi wa miradi mipya, na ukarabati na upanuzi wa miradi iliyopo. Jamii pia itatakiwa kuchangia nguvu kazi kwenye miradi hiyo. Uungaji wa maji majumbani utaruhusiwa pale ambapo maji yaliyopo yanakidhi kiwango cha chini cha huduma ya maji. Gharama zote za uunganishaji zitabebwa na wale watakaohitaji kupata huduma hiyo majumbani mwao. Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za wananchi kwa kutafuta na kutoa msaada wa fedha.

Ili kuwawezesha wananchi kushiriki katika kugharamia miradi yao ya maji, yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Utaratibu wa wananchi kubuni mradi na kisha kuomba msaada, badala ya wananchi kupelekewa mradi ambao kwao siyo kipaumbele utatumika.



- (ii) Wananchi watajiwekea utaratibu wa kuchangia, kwa fedha taslimu na nguvu kazi, kwa ajili ya ujenzi wa miradi mipya, ukarabati na upanuzi wa miradi iliyopo.
- (iii) Wananchi watajipangia utaratibu wa kulipia gharama zote za uendeshaji na matengenezo.
- (iv) Maeneo yenye uhaba wa maji yataainishwa na kupewa kipaumbele kulingana na umuhimu wake.

4.11 Taratibu za Uendeshaji Miradi Kisheria

Lengo: Wananchi kuendesha miradi yao ya maji kisheria.

Serikali, mashirika ya kimataifa pamoja na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, kwa muda mrefu yamekuwa yakipanga, kujenga na kuendesha miradi ya maji vijijini bila kushirikisha wananchi kikamilifu. Serikali imekuwa ndiyo mmiliki na mwendeshaji wa miradi ya maji vijijini, jambo ambalo limefanya wananchi waone kuwa miradi hiyo si yao, na hivyo kutoona umuhimu wa kuitunza na kuilinda. Masuala ya miliki na usimamizi wa miradi katika ngazi ya watumiaji maji ni ya msingi kabisa ili kufanya miradi hiyo iwe endelevu. Kwa kutambua hilo, miradi iliyopo pamoja na itakayojengwa, itamilikiwa kisheria na kuendeshwa na vyombo husika vya watumiaji wa maji. Aidha, kanuni na taratibu zitawekwa ili kuhakikisha kuwa kila chombo kinafuata viwango vilivyowekwa vya utoaji wa huduma.

Ili kuboresha taratibu za uendeshaji miradi ya maji kisheria, yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Sheria na taratibu za kusajili vyombo vya watumia maji zitafanyiwa mapitio.
- (ii) Kanuni mbalimbali zitaandaliwa ili kutumiwa na wadau, ikiwa ni pamoja na sekta binafsi, katika kuendesha miradi ya maji vijijini.
- (iii) Taarifa kuhusu kanuni mbalimbali zinazotawala usimamizi na utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini, zitasambazwa kwa wadau wote.

4.12 Mfumo wa Kitaasisi

Lengo: Kuwa na mfumo wa kitaasisi unaokidhi hali halisi.

Ili huduma ya maji na usafi wa mazingira iwe endelevu, itabidi wananchi wawe mstari wa mbele katika kubuni na kujenga miradi yao ya maji na kuwajibika kikamilifu katika uendeshaji na matengenezo. Sekta Binafsi itasaidia wananchi kupanga, kusanifu na kujenga miradi, pamoja na upatikanaji wa vifaa vya ujenzi, mitambo na vipuli mbalimbali. Serikali itaendelea kutoa msaada wa kiufundi na kifedha, pamoja na kuratibu na kusimamia upatikanaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira. Mashirika ya kimataifa na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yatatoa misaada ya kiufundi pamoja na kifedha. Ili mipango ya uwiano ya huduma za maji, usafi wa mazingira na elimu ya afya iwe mizuri, itabidi kuwe na ushirikiano wa karibu zaidi na watekelezaji wengine katika sekta ya usafi wa mazingira na elimu ya afya.

Utaratibu huu mpya unahitaji mfumo bora wa kitaasisi unaonesha waziwazi mahusiano yote kati ya makundi makuu ya watekelezaji katika sekta ya maji, usafi wa mazingira na elimu ya afya, ikiwa ni pamoja na Serikali Kuu, Halmashauri za Wilaya, Mashirika ya Kimataifa yanayotoa misaada, Sekta Binafsi, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, jumuiya mbalimbali za wananchi vijijini, na wananchi wenyewe.

Mfumo wa kitaasisi ambao ni rahisi, ulio wazi, wenye kuleta ufanisi na ambao unaonesha uwajibikaji kwa wananchi utawekwa, ili kuwezesha miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini kuwa endelevu. Majukumu na wajibu wa watekelezaji mbalimbali yataoneshwa bayana. Aidha, mahusiano na taratibu za ushirikiano za watekelezaji zitawekwa na kuratibiwa kikamilifu, na masuala yote kwa ujumla yataratibiwa na kufanyiwa tathmini ili kupata uzoefu utakaosaidia kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini.



Ili kufanikisha shughuli hii yafuatayo yatafanyika:

- (i) Mfumo wa kitaasisi uliopo utarekebisha ili ulingane na wajibu na majukumu mapya.
- (ii) Wajibu na majukumu ya kila mtekelezaji kwenye utoaji wa huduma ya maji vijijini, yatawekwa bayana na kusambazwa.
- (iii) Utaratibu wa ushirikiano miongoni mwa wadau utandaliwa.
- (iv) Mfumo wa kuleta pamoja watekelezaji wote wakuu ili kujadili na kubadilishana mawazo kuhusu uzoefu wao na kusaidia kuratibu shughuli mbalimbali za maji vijijini, utawekwa.
- (v) Wananchi watahamasishwa kuhusu wajibu na majukumu yao.

4.13 Uratibu na Ushirikiano

Lengo: Kuwa na mfumo madhubuti wa uratibu na ushirikiano katika utoaji huduma ya maji vijijini.

Taratibu zilizopo za uratibu na ushirikiano miongoni mwa watekelezaji mbalimbali wanaotoa huduma ya maji vijijini, zinahusu miradi husika. Kwa hali hii, uzoefu unaopatikana kwenye miradi mbalimbali nchini hausambazwi kwa watekelezaji wengine. Ni muhimu kuhakikisha kuwa wadau wanayajua matatizo, mafanikio na mahitaji ya sekta hii, ili kubadilishana uzoefu kwa lengo la kuandaa mipango ya pamoja. Ukosefu wa uratibu na ushirikiano husababisha kurudia utekelezaji wa shughuli ambazo tayari zimekwisha fanyika, na hivyo kusababisha matumizi mabaya ya rasilimali zilizopo. Aidha, taratibu tofauti zinazotumiwa na watekelezaji mbalimbali huchanganya mawazo wananchi.

Taratibu zinazostahili kwa ajili ya uratibu na ushirikiano miongoni mwa vyombo vya watumiaji maji na wadau mbalimbali zitawekwa bayana na kuimarishwa.

4.14 Ufuatiliaji na Tathmini

Lengo: Kuwa na mfumo mzuri wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maji.

Uboreshaji wa utoaji huduma ya maji unahitaji kufuatiliwa na kufanyiwa tathmini za mara kwa mara kwa lengo la kupata uzoefu kuhusu miradi inavyoendeshwa sehemu mbalimbali nchini. Ushiriki wa walengwa katika ufuatiliaji na tathmini utafanywa katika ngazi ya Wilaya na Kijiji, kwa kusaidiwa na Serikali Kuu, Halmashauri za Wilaya, Mashirika ya Kimataifa yanayotoa misaada, Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali, na Sekta Binafsi. Ushiriki wa watekelezaji wote wakuu na makundi mengine yanayohusika katika ufuatiliaji utahimizwa.

Ili kuwa na mfumo mzuri wa ufuatiliaji na tathmini, yafuatayo yatafanywa:

- (i) Uwezo wa wananchi kufuatilia miradi yao kitaalam utajengwa na kuimarishwa.
- (ii) Benki za takwimu, zinazoendeshwa kwa kutumia kompyuta, zitaanzishwa kwenye ngazi za Wilaya na Taifa.
- (iii) Utaratibu madhubuti wa kupeana taarifa katika kila ngazi utawekwa.

SEHEMU III: HUDUMA YA MAJISAFI NA MAJITAKA MIJINI



1. MAELEZO YA JUMLA

Miji mingi nchini inakua kwa kasi kubwa. Idadi ya watu inaongezeka kwa zaidi ya 6% kwa mwaka na hivyo kusababisha ongezeko la haraka la mahitaji ya huduma mbalimbali zikiwemo zile za majisafi na majitaka. Aidha, inakadiriwa kuwa kati ya theluthi moja hadi nusu ya wakazi wote mijini wanaishi kwenye maeneo yasiyopimwa na yenye huduma zisizoridhisha. Maeneo haya yana nyumba za hali duni na msongamano mkubwa wa watu na yanakosa miundombinu ya huduma mbalimbali ikiwemo ya maji na usafi wa mazingira.

Inakadiriwa kuwa 73% ya wakazi mijini wanapata huduma ya majisafi na chini ya 10% wanapata huduma ya uondoaji majitaka. Aidha, miundombinu iliyopo ni ya siku nyingi, imechakaa na haifanyi kazi ipasavyo.

Masuala na changamoto ya msingi katika utoaji wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka ni pamoja na usambazaji wa maji yasiyokidhi viwango vya ubora unaotakiwa na yasiyotosheleza mahitaji. Aidha, utayarishaji wa ankara za maji na ukusanyaji wa maduhuli una udhaifu mkubwa. Matatizo mengine ni kukosekana kwa mazingira mazuri ya kuiwezesha Sekta Binafsi kuwekeza kwenye huduma ya majisafi na majitaka, na pia wananchi walio wengi kuendelea kuamini kuwa maji ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu isiyokuwa na thamani na hivyo inastahili kutolewa bure.

2. MADHUMUNI

Madhumuni ya Sera hii ni kuwezesha uendelezaji na usimamizi endelevu wa utoaji wa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka kwa wakazi wa mijini. Madhumuni hayo yatafikiwa kwa kuweka malengo na kutoa miongozo na vigezo vya utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini na watekelezaji wengine, kwa nia ya kuboresha huduma ya utoaji majisafi na uondoaji majitaka mijini. Aidha, Sera inalenga katika masuala yafuatayo:

- (i) Kutoa mwongozo wa namna ya kuendeleza na kusimamia huduma ya majisafi na majitaka mijini kwa ufanisi.
- (ii) Kuweka mazingira mazuri yatakayoivutia Sekta Binafsi kuwekeza katika kutoa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini.
- (iii) Kuhakikisha kuwa upo muundo mzuri wa kitaasisi unaovipa vyombo vya uendeshaji huduma ya majisafi na majitaka mijini madaraka ya kujiendesha vyenyewe kibiashara.
- (iv) Kuwa na mfumo madhubuti na wenye ufanisi wa ukusanyaji maduhuli yatokanayo na mauzo ya majisafi na uondoaji wa majitaka na hivyo kuongeza mapato.
- (v) Kupunguza upotevu wa maji na kuboresha uondoaji wa majitaka.

3. MISINGI

Mapungufu na changamoto zilizojitokeza katika utoaji wa huduma ya utoaji majisafi na uondoaji majitaka unahitaji msisitizo katika kuboresha usimamizi wa huduma hiyo kwa misingi ya mfumo madhubuti wa usimamizi wa huduma hiyo. Utaratibu utakaotumika utafuata misingi kadhaa ambayo inatokana na vikao mbalimbali vya wadau na uzoefu uliopatikanika katika kutekeleza Sera ya Maji ya 1991.

Kwa upande wa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini, Sera hii imejengeka katika misingi ifuatayo:



- (i) Majisafi na usafi wa mazingira ni muhimu kwa maendeleo na hivyo ni haki ya kila mwananchi kupatiwa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka.
- (ii) Udhibiti wa ubora wa huduma zitolewazo ni muhimu.
- (iii) Ulipiaji gharama zote za utoaji na uendelezaji wa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini ndio mhimili mkuu wa kuhakikisha kuwa huduma hii inakuwa endelevu.
- (iv) Ni wajibu wa wakazi wote mijini kulipia gharama zote za kuondoa na kusafisha majitaka wanayozalisha kulingana na kiasi cha maji wanayotumia.
- (v) Msisitizo mkubwa utawekwa kwenye kudhibiti matumizi ya maji na kuzuia upotevu.
- (vi) Wakazi wenye kipato kidogo mijini watafikiriwa wakati wa kuweka mtandao wa kusambaza maji na kupanga bei za maji.
- (vii) Huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini itaendeshwa na vyombo vinavyojitegemea na vilivyo karibu na walengwa.
- (viii) Uendelezaji wa huduma ya majisafi na majitaka utasimamiwa kwa pamoja.
- (ix) Sekta Binafsi itawekwa mazingira mazuri ya kuwekeza na kuendesha huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini.
- (x) Uhusiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi utaboreshwa na kuendelezwa kadiri iwezekanakavyo.
- (xi) Mfumo wa kisheria wa usimamizi utakuwa huru, wa uwazi na wa haki kwa wote.
- (xii) Tathmini ya athari katika mazingira itakuwa ni ya lazima katika kuandaa miradi mipya ya majisafi na majitaka.

4. MASUALA YA SERA KUHUSU MAJISAFI NA MAJITAKA MIJINI

4.1 Vyanzo vya Maji na Miundombinu ya Maji

Uchakavu wa miundombinu

Lengo: Kukarabati na kupanua miundombinu ya kutoa huduma ya majisafi na majitaka ili iweze kutoa huduma endelevu.

Miundombinu ya majisafi na majitaka katika miji mingi imechakaa na haina uwezo wa kutoa huduma ya kutosheleza ongezeko kubwa la mahitaji, yakiwemo ya dharura kama vile huduma ya kuzima moto. Matokeo ya hali hii ni kuwa maji yanayotolewa mara nyingi hayatoshelezi mahitaji na hayana ubora wa kutosha. Aidha, huduma ya kuondoa na kusafisha majitaka ili kulinda mazingira na afya za wananchi ni ya kiwango cha chini sana. Mikakati itawekwa ili kuhakikisha kuwa nyakati za ukame, mafuriko na majanga ya moto, maji yanapatikana.

Ili kuwa na miundombinu yenye uwezo wa kutoa huduma yenye ufanisi na endelevu yafuatayo yatafanyika:

- (i) Serikali itatafuta fedha za kuwekeza kwenye ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka mijini.
- (ii) Upanuzi na ukarabati wa miradi ya majisafi utafanyika sambamba na miradi ya majitaka kwa kuzingatia usafi wa mazingira.
- (iii) Mamlaka za maji zitatayarisha mipango ya kutenga fedha kwa ajili ya kukabiliana na majanga mbalimbali.
- (iv) Taratibu za kukabiliana na majanga ya ukame, mafuriko na moto zitatayarishwa ili kutumika.
- (v) Wakati wa upungufu mkubwa wa maji au migogoro ya maji, maji kwa matumizi ya binadamu na kwa matumizi ya dharura yatapelelewa umuhimu wa kwanza.

Uvamizi wa maeneo ya vyanzo vya maji

Lengo: Kulinda vyanzo vya maji kutokana na uvamizi wa ardhi kwenye maeneo ya vyanzo hivyo.



Katika miaka ya hivi karibuni, shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi zimeleta athari katika mazingira. Vyanzo vya maji vinachafuliwa na majitaka kutoka majumbani na viwandani, mbolea za chumvi chumvi na madawa ya kilimo, na mmomonyoko wa ardhi. Uvamizi wa ardhi kwenye maeneo ya vyanzo vya maji unazidi kuongezeka siku hadi siku kutokana na maeneo hayo kutopimwa na kupewa hati miliki ya ardhi. Ili kukabiliana hali hii:

- (i) Maeneo yenye vyanzo vya maji yatakimwa na kupewa hati miliki ya ardhi.
- (ii) Miundombinu mikubwa itaainishwa na kupatiwa hakimiliki na hatinjia.
- (iii) Sheria za kulinda miundombinu muhimu kama mabwawa, mabomba, mitambo ya kusafisha maji, vituo vya kusukuma maji, matanki ya maji na miliki nyingine kama zilivyotamkwa kwenye Sheria za Miji pamoja na sheria nyingine, pia zitatajwa kwenye Sheria za Maji ili kurahisisha utekelezaji na usimamizi wa Sheria za maji.
- (iv) Tathmini ya kina kuhusu umiliki wa ardhi husika itafanyika kabla ya kuomba hati za kutumia vyanzo vya maji. Aidha, taratibu za kumilikisha miundombinu kwa mamlaka za maji zitakamilishwa.

Viwango vya ujenzi, uendeshaji wa miradi na ubora wa maji

Lengo: Kudhibiti ubora wa viwango vya ujenzi, uendeshaji wa miradi na ubora wa maji.

Kwa vile sasa Sekta Binafsi itashiriki katika kutoa huduma ya majisafi na majitaka mijini, watoa huduma hii wataongezeka na hivyo miongozo ya utendaji wa kazi haina budi kutayarishwa. Miundombinu ya majisafi na majitaka itaendeshwa kwa mapato yatokanayo na malipo ya huduma hiyo. Usanifu wa mifumo ya majisafi na majitaka utazingatia matakwa na mahitaji ya watumiaji wa huduma hiyo. Aidha, usanifu wa miradi utazingatia miongozo inayotolewa na Wizara inayohusika na maji na viwango vinavyokubalika kimataifa.

Ili kuhakikisha ubora wa huduma ya maji:

- (i) Viwango vya ubora wa mashine za kusukuma maji, madawa na mitambo ya kusafishia majisafi na majitaka vitatayarishwa.
- (ii) Miongozo inayohusu usanifu wa miradi ya majisafi na majitaka itafanyiwa mapitio na kusambazwa.
- (iii) Wafanyakazi wa Mamlaka za Maji wataandaliwa mafunzo ili kuboresha utendaji wao wa kazi.
- (iv) Vyombo vinavyotoa huduma ya maji mijini vitatakiwa kupima ubora wa maji mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa ni safi na salama kwa matumizi ya binadamu.
- (v) Mamlaka za maji zitahakikisha kuwa majisafi yanakuwa na ubora unaokubalika kulingana na viwango vilivyowekwa.

4.2 Uwekezaji na Ulipiaji Maji

Ulipiaji usiokidhi gharama za kutoa huduma ya maji

Lengo: Kuhakikisha kuwa wanaotumia huduma ya majisafi na majitaka mijini wanalipia gharama zote za kutoa huduma hiyo.

Kwa kipindi kirefu sasa, wananchi wamekuwa wanapatiwa huduma ya majisafi na majitaka kwa bei ya chini isiyokidhi gharama halisi. Hii imefanya waone kuwa jukumu la kutoa na kugharamia huduma hii ni la Serikali Kuu. Hali hii imefanya kazi ya kukusanya maduhuli kuwa ngumu. Wananchi wengi wanakataa hata kuunganishiwa maji kihalali, na wale wenye akaunti wanakuwa wazito kulipia ankara za maji. Mamlaka za Maji Mijini zimeendelea kuwa na udhaifu katika kutayarisha bili, kukusanya maduhuli, kuwafungia wateja mita za maji na hata



kudhibiti uvujaji na matumizi mabaya ya maji. Maendeleo ya huduma ya majisafi na majitaka mijini, yatapatikana kutokana na wenye kunufaika na huduma hiyo kuilipia kikamilifu.

Ili kuhakikisha kuwa wanaonufaika na huduma ya majisafi na majitaka wanalipia huduma hiyo yafuatayo yatafanyika:

- (i) Watumiaji wote wa maji watatakiwa kulipia huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka wanayoipata.
- (ii) Taratibu nzuri za kupanga na kudhibiti bei za maji kwa kuzingatia gharama zote za utoaji huduma zitatayarishwa.
- (iii) Wananchi wataelimishwa taratibu na sababu za kupanga na kubadilisha bei za maji.
- (iv) Programu ya kuwafungia wateja wote mita za maji na kuunganisha kwenye mifumo ya mabomba ya majisafi na uondoaji majitaka itawekwa na kutekelezwa.
- (v) Utaratibu utawekwa wa kila nyumba iliyopo umbali usiozidi mita 30 kutoka bomba la majitaka kuunganishwa kwenye bomba hilo kwa gharama nafuu.
- (vi) Pale ambapo maji yanapatikana, utaratibu utawekwa wa kufanya gharama za kuunganisha maji kwenye nyumba kuwa nafuu ili kila nyumba iunganishwe kwenye bomba la maji.
- (vii) Vyanzo vya maji vya binafsi havitaruhusiwa katika eneo la mji isipokuwa kwa ruhusa ya Mdhibiti aliyeruhusiwa kisheria.

Uwezo mdogo wa kifedha kwa ajili ya kutoa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini

Lengo: Kuvutia uwekezaji katika kutoa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini.

Fedha zinazotengwa kwa baadhi ya Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini kwa ajili ya uwekezaji, uendeshaji na matengenezo hazitoshi. Hali hii inasababisha kutokuwa na huduma endelevu ya majisafi na uondoaji majitaka mijini inayokidhi mahitaji. Aidha, hali hii inazifanya mamlaka za maji mijini zisimudu kujiendesha kibiashara na hivyo kutovutia wawekezaji mbalimbali.

Kwa kuelewa kuwa majitaka yasipoondolewa mijini na kusafishwa vizuri yanaweza kusababisha magonjwa, na kwa vile majitaka ya mkazi mmoja yanaweza kusababisha kuenea magonjwa mji mzima, upo umuhimu wa kuhakikisha kuwa majitaka yanakusanywa, yanasafishwa na kurudishwa kwenye mikondo ya maji bila kuathiri mazingira na afya za watu. Kwa mantiki hiyo uwekezaji katika upanuzi, uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya majisafi, utaenda sambasamba na ule wa miundombinu ya majitaka kwa kuweka uwiano katika huduma hizi mbili.

Ili kuvutia uwekezaji katika kutoa huduma ya majisafi na majitaka mijini yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji yatawekwa.
- (ii) Fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje zitatafutwa kwa ajili ya kugharamia ukarabati na upanuzi wa miundombinu ili kuzifanya mamlaka zote za maji mijini ziweze kujiendesha kibiashara na hivyo kuvutia wawekezaji mbalimbali.
- (iii) Utaratibu utawekwa ili magari ya majitaka yasitowezwa ada ya kumwaga majitaka kwenye mabwawa ya kusafishia majitaka hayo.

4.3 Udhhibiti wa Matumizi ya Maji

Lengo: Kudhibiti matumizi ya maji na kuzuia upotevu na wizi wa maji



Mahitaji ya maji mijini yanaongezeka kwa kasi isiyolingana na upanuzi wa huduma ya majisafi na majitaka. Hii inatokana na ongezeko la watu mijini, uzalishaji wa viwandani na kiwango kikubwa cha upotevu wa maji na wizi wa maji. Hivyo, ipo haja ya kutumia vizuri maji kidogo yaliyopo. Ili kudhibiti hali hii yafuatayo yatafanyika:

- (i) Upangaji mzuri wa bei za maji, uwekaji wa mita, mgao wa maji, udhibiti wa uvujaji na elimu kwa wananchi vitafanywa ili maji yatumike vizuri.
- (ii) Sheria na taratibu zinazohimiza matumizi ya maji kwa uangalifu ikiwa ni pamoja na matumizi ya vyoo vinavyotumia maji kidogo, zitaandaliwa ili kutumika.

4.4 Maji kwa Wakazi Wenye Kipato Kidogo

Lengo: Kuwa na huduma ya majisafi na majitaka katika maeneo yenye wakazi wenye kipato kidogo na maeneo yasiyopimwa pembezoni mwa miji.

Kwa kawaida, wakazi waishio maeneo yenye makazi duni, watu wenye kipato kidogo, pamoja na waishio pembezoni mwa miji, hawapati huduma nzuri ya majisafi na majitaka. Wanahunua maji kutoka kwenye vituo au kwa wauza maji kwa bei kubwa kuliko wale waliunganishiwa maji majumbani mwao. Maeneo ya makazi duni mijini yanaweza kuwa chanzo cha milipuko ya magonjwa mengi mijini. Sera hii inasisitiza kuwa wakazi hawa lazima watambuliwe na wapatiwe huduma ya majisafi na majitaka, na kwa bei nafuu. Aidha, katika kuikaribisha Sekta Binafsi, ambayo lengo lake kuu ni kutoa huduma kwa faida, haki na mahitaji ya wakazi hawa lazima yazingatiwe katika mikataba mbalimbali itakayosainiwa.

Ili kuwa na huduma ya majisafi na majitaka katika maeneo yenye wakazi wenye kipato kidogo na maeneo yasiyopimwa pembezoni mwa miji yafuatayo yatafanyika:

- (i) Mipango na mikakati itawekwa ya kuwapatia huduma ya majisafi na uondoaji majitaka katika maeneo yasiyopimwa na pembezoni mwa miji.
- (ii) Elimu itatolewa kuhusu matumizi ya majisafi na salama.
- (iii) Mifumo ya majitaka inayotumia mabomba yenye vipenyo vidogo na ambayo hayahitaji mitaro ya kina kirefu itaendelezwa.
- (iv) Ushirikishaji wa Sekta Binafsi katika kutoa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini utazingatia meneo yasiyopimwa na yaliyo pembezoni mwa miji.
- (v) Mashirika yasiyo ya kiserikali na yale ya wananchi yatahimizwa kuwekeza na kuendeleza huduma ya maji na usafi wa mazingira, katika maeneo duni, yasiyopimwa na yale ya pembezoni mwa miji.

4.5 Majitaka na Mazingira

Kusimamia huduma ya majitaka ili isiathiri mazingira.

Lengo: Kuwa na mfumo wa kusimamia undoaji majitaka usioathiri mazingira.

Asilimia 80 ya majisafi yote yatumikayo mijini hubadilika kuwa majitaka ambayo hutakiwa kuondolewa na kusafishwa kabla ya kumwagwa kwenye mito, maziwa au bahari. Hata hivyo, majitaka yanayozalishwa mijini hayaondolewi na kusafishwa ipasavyo. Wakazi wengi hutumia njia za vyoo vya shimo na matanki ya maji machafu, na hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kuchafua mazingira na hasa maji chini ya ardhi. Ni jukumu la kila chombo cha usimamizi na utoaji wa huduma ya majisafi na majitaka mjini kuhakikisha kuwa, majitaka yanakusanywa, yanaondolewa na kusafishwa ipasavyo kabla ya kumwagwa mtoni, ziwani au baharini. Upelekaji wa majitaka baharini kwa kutumia mifereji ya wazi hautakubalika kwani unachafua fukwe.

Viwanda vingi vilijengwa bila kuwa na mitambo ya kusafisha majitaka, na wakati huohuo majitaka kutoka viwanda yana kemikali na vijimelea vinavyozuia usafishwaji mzuri. Viwanda vitahimizwa kutumia teknolojia za kisasa zinazopunguza wingi wa majitaka. Aidha, mamlaka mbalimbali za kutoa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini vitatakiwa kupima ubora wa majitaka kila mara na hasa ubora wa majitaka kutoka viwandani, kabla hayajapelekwa kwenye mitambo au mabwawa ya kusafishia majitaka.

Ili huduma ya majitaka kutoka majumbani na viwandani isiathiri mazingira yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Mifumo ya uondoaji majitaka itajengwa na ile ambayo ipo itakarabatiwa.
- (ii) Unyonyaji wa majitaka kwa kutumia magari utahimizwa na Sekta Binafsi itashirikishwa kikamilifu. Aidha, magari hayo yatadhibitiwa yasimwage majitaka ovyo au kwenye chemba za njia za majitaka badala yake yamwage kwenye maeneo mahsusi ya kusafishia majitaka.
- (iii) Umwagaji majitaka baharini utafanywa kwa kutumia mabomba yenye urefu wa kutosha kuweza kufikisha majitaka kwenye kina kirefu cha bahari.
- (iv) Sheria zinazovitaka viwanda kusafisha majitaka yao kabla ya kupelekwa kwenye mitambo ya kusafishia majitaka zitafanyiwa mapitio na utekelezaji wake utawekewa mkazo zaidi.
- (v) Mamlaka za maji zitashirikiana na viwanda katika kufanya utafiti wa teknolojia nafuu za kusafisha majitaka na kuyatumia tena.
- (vi) Viwanda vitatakiwa kutotumia teknolojia na malighafi zinazochangia kuharibu mazingira.
- (vii) Mamlaka za maji zitahakikisha kuwa majitaka yanayomwagwa kwenye mito na maziwa yana ubora unaokubalika baada ya kusafishwa.

4.6 Mfumo wa Kitaasisi

Lengo: Kuwa na mfumo wa kitaasisi ulio kamili na wenye ufanisi.

Kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, Serikali sasa haitatoa huduma mbalimbali kwa wananchi moja kwa moja bali huduma hizo zitatolewa na vyombo vingine katika ngazi husika. Vyombo hivyo vitapewa uhuru na madaraka ya kujiendesha vyenyewe kwa mujibu wa Sheria. Serikali itabaki na jukumu la kuwezesha huduma kutolewa kwa ubora na ufanisi zaidi pamoja na kuwekeza katika sekta.

Ili kuwa na muundo wenye ufanisi katika kutoa huduma ya maji:

- (i) Majukumu ya Wizara inayohusika na maji yatarekebishwa na uwezo wa Mamlaka za maji mijini kutoa huduma utaimarishwa.
- (ii) Vikundi vya watumiaji maji na ushiriki wa Sekta Binafsi vitaendelezwa.
- (iii) Wafanyakazi katika ngazi zote watapatiwa mafunzo zaidi.
- (iv) Utaratibu mahsusi wa kusimamia na kutathmini utendaji wa mamlaka mbalimbali katika utoaji huduma mijini utawekwa.

4.7 Mfumo wa Kisheria

Lengo: Kuwa na mfumo wa sheria ulio kamili unaosimamia utoaji huduma ya majisafi na majitaka mijini.

Sheria za maji zilizopo sasa zilitungwa nyakati mbalimbali katika miaka iliyopita. Aidha, baadhi ya Sheria zipo nje ya Wizara inayohusika na maji na zinakingana na Sheria za maji ndani ya Wizara. Masuala mengine muhimu katika sekta hayana Sheria kamilifu za kuyasimamia. Sheria hizi zitafanyiwa mapitio na kuoanishwa na zile zilizopo nje ya Wizara.



Ushiriki wa Sekta Binafsi katika kutoa huduma ya majisafi na uondoaji wa maji mijini unaweza kusababisha ongezeko la bei na migogoro iwapo hakutakuwepo na udhibiti mzuri. Ni wazi kuwa upo uwezekano mkubwa wa kutokea migongano kati ya watumiaji wa maji na mwendeshaji wa miundombinu husika. Msimamizi na Mdhibiti mwenye madaraka ya kisheria atawekwa ili kushughulikia na kupunguza migogoro ya aina hii. Aidha, uanzishaji wa chombo kipya cha usimamizi na udhibiti wa utoaji huduma za jamii (EWURA – Energy and Water Utilities Regulatory Authority) umeweka misingi ya kumpata Msimamizi na Mdhibiti katika Sekta ya Maji Mijini. Jukumu la msingi la Serikali kupitia Wizara husika litakuwa ni kusimamia na kudhibiti sekta zisizodhibitiwa na EWURA, kuweka viwango mbalimbali na kupima mafanikio na matatizo ya mfumo huu mpya wa kutoa huduma mijini.

Ili kuwa na usimamizi na udhibiti kamili wa utoaji huduma ya majisafi na majitaka mijini, yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Sheria zinazohusu huduma za maji mijini zitasisitiza kufidia gharama za uharibifu badala ya faini pekee.
- (ii) Sheria zinazohusu huduma za maji mijini zitafanyiwa mapitio na zile zinazopingana zitarekebishwa na kuwekwa pamoja.
- (iii) Sheria za maji zitatafsiriwa kwa Kiswahili ili ziweze kueleweka kwa watu walio wengi.

4.8 Sekta Binafsi

Lengo: Kuwa na ufanisi katika utoji wa huduma ya majisafi na majitaka mijini kwa kuishirikisha Sekta Binafsi.

Ni jukumu la Serikali kuweka mazingira mazuri ya kuiwezesha Sekta Binafsi, wakiwemo wazalendo, kuwekeza na kutoa huduma ya majisafi na majitaka. Miundombinu iliyopo itafanyiwa ukarabati na upanuzi ili kuboresha huduma na kuvutia Sekta Binafsi. Aidha, mwekezaji ataruhusiwa kuwekeza kwenye zaidi ya mji mmoja bila kuleta ukiritimba kama kufanya hivyo kutapunguza gharama za uendeshaji. Kwa nia ya kuhamasisha uwekezaji na kupunguza gharama za uendeshaji na matengenezo, chombo kimoja cha kumiliki mali katika miji kadhaa kinaweza kuundwa.

Sekta Binafsi itakaribishwa kuwekeza kwenye sekta ya maji. Aidha, Serikali itaweka mazingira mazuri ya kuiwezesha Sekta Binafsi kuwekeza na yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Mamlaka za majisafi na majitaka zitaimarishwa kwa ajili ya kuivutia Sekta Binafsi.
- (ii) Uwezo wa Wizara inayohusika na maji kuweka mazingira ya kuwavutia na kuwapata wakezaji binafsi katika uendeshaji, uuzaji wa vifaa na utoaji huduma mbalimbali zinazohusiana na majisafi na majitaka mijini utaimairishwa
- (iii) Kampeni za kuelimisha jamii kuhusu madhumuni na faida za kushirikisha Sekta Binafsi zitafanywa.
- (iv) Sekta Binafsi ya hapa nchini itaimarishwa.
- (v) Watoa huduma wadogo wadogo katika utoaji wa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka wataainishwa na kutambuliwa rasmi.
- (vi) Taratibu zitawekwa kuiwezesha Serikali kufanya tathmini ya mara kwa mara ili kujua utendaji wa kazi wa Sekta Binafsi katika utoaji huduma ya majisafi na majitaka mijini.

4.9 Ubinafsishaji wa Huduma ya Majisafi na Majitaka Kwenye Miji Midogo

Lengo: Kuwa na huduma ya majisafi na majitaka iliyo na ufanisi, kwenye miji midogo.

Hadi sasa, msisitizo mkubwa umekuwa kwenye kuboresha huduma ya majisafi na majitaka kwenye miji mikuu ya mkoa. Miji midogo nayo sasa itapewa kipaumbele kwa kuruhusu



uanzishaji wa vyombo huru vya kutoa huduma ya majisafi na majitaka kwenye miji hiyo. Ili kufanikisha haya:

- (i) Mkazo utawekwa katika ubinafsishaji wa huduma ya majisafi na majitaka kwenye miji midogo, ambapo makampuni binafsi yatakaribishwa.
- (ii) Sekta Binafsi ya hapa nchini itaimarishwa na kuwezesha.

4.10 Ufuatiliaji na Tathmini

Lengo: Kuwa na mamlaka zenye uwezo wa ufuatiliaji na tathmini ya utoaji huduma ya majisafi na majitaka mijini.

Ufuatiliaji wenye lengo la kuchambua, kutathmini, kupitia na kupima utendaji unasaidia katika usimamizi madhubuti wa taasisi husika. Hivi sasa, Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini zina uwezo mdogo wa ufuatiliaji wa utoaji huduma. Aidha, mifumo ya taarifa za menejimenti katika mamlaka hizo haikidhi hali halisi. Kwa mfano, utunzaji na usambazaji takwimu na taarifa zilizokusanywa kwa njia mbalimbali hauridhishi, kwani takwimu na taarifa hizo bado zimo katika mafaili ya karatasi ingawaje hii ni karne ya kompyuta.

Ili kuwa na ufanisi katika ufuatiliaji na tathmini ya utoaji huduma ya majisafi na majitaka mijini yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) Miongozo ya utendaji kazi iliyopo itaboreshwa na viashiria vya utendaji vitaanishwa.
- (ii) Uwezo wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini kutenda kazi zake utaimarishwa.
- (iii) Benki za takwimu zinazohusika na utoaji huduma, zitaanzishwa katika ngazi mbalimbali.
- (iv) Mfumo muafaka wa kupeana taarifa utatayarishwa ili kubaini ufanisi wa utendaji kazi katika nyanja za kiufundi, kifedha na kiutawala.

4.11 Uwajibikaji kwa Umma

Lengo: Kuwa na vyombo vya kutoa huduma ya majisafi na majitaka vinavyowajibika kwa wateja wao.

Katika kutoa huduma ya majisafi na majitaka kwa wananchi mijini, vyombo husika ni lazima viwajibike kwa watumiaji wa huduma hiyo. Wananchi wapatiwe huduma nzuri kwa bei nafuu na wawe na sauti katika masuala yahasuyo maji. Kwa upande wa wananchi, nao wawe tayari kulipia ankara za majisafi na majitaka mapema, watumie maji kwa uangalifu na wawe walinzi wazuri wa miundombinu inayowapatia huduma hiyo. Taratibu zitawekwa za kuhakikisha kuwa vyombo vya kutoa huduma vinawajibika kwa wananchi na kuwa nao pia wanaitikia kwa kutimiza yale yote yanayowahusu, na hivyo:

- (i) Utaratibu wa mawasiliano na kupashana habari mara kwa mara kati ya Mamlaka za Majitaka na Majisafi Mijini, wadau na wananchi kwa jumla utaimarishwa.
- (ii) Taratibu za ulinzi wa miundombinu kwa kuwashirikisha wananchi zitabuniwa.
- (iii) Wananchi watahamasishwa, wataelimishwa na kushirikishwa katika utunzaji na upunguzaji wa matumizi mabaya ya maji.

4.12 Kujenga Uwezo

Lengo: Kuwa na huduma ya majisafi na majitaka ambayo ni endelevu na yenye ufanisi.

Huduma endelevu ya majisafi na majitaka mijini inahitaji kuwepo kwa uwezo wa kutosha wa wafanyakazi, vifaa, vyombo na miundombinu ya kufanyia kazi. Ipo haja ya huduma hii kutolewa na chombo chenye uwezo, kilichoundwa kisheria na kinachojitegemea. Serikali



itahakikisha kuwa wafanyakazi wanaotoa huduma ya majisafi na majitaka wanakuwa na utaalamu na uzoefu wa kutosha. Aidha, wanawake watawezesha kufikia ngazi za juu za kitaaluma na kiutawala.

Huduma endelevu mijini zitategemea Mamlaka imara zenye wafanyakazi wenye uwezo wa hali ya juu. Hivyo basi:

- (i) Mamlaka zitapatiwa vitendea kazi vya kutosha na miundombinu iliyopo itapanuliwa.
- (ii) Utaalamu uliopo utaendelezwa.
- (iii) Programu ya mafunzo itatayarishwa.
- (iv) Mpango wa kujaza nafasi za fani mbalimbali utaandaliwa na kutekelezwa ili kuepuka upungufu wa wataalam wakati wowote ule.

4.13 Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia

Lengo: Kuimarisha utafiti na matumizi ya teknolojia mpya.

Teknolojia zinazotumika katika Sekta ya Maji ni nyingi na teknolojia mpya zenye ufanisi zaidi zinajitokeza siku hadi siku. Aidha, matatizo ambayo yangeweza kupatiwa ufumbuzi wa kiteknolojia ni mengi. Serikali itahakikisha kuwa utafiti unafanyika kuhusu teknolojia nafuu ambazo zitaweza kusaidia uboreshaji wa huduma na kwa gharama nafuu, kwa kufanya yafuatayo:

- (i) Uhusiano kati ya wadau wa sekta na vituo vya utafiti vya kimataifa utaboreshwa.
- (ii) Taratibu za mawasiliano kuhusu utafiti katika sekta zitaimarishwa.
- (iii) Utafiti utakofanywa na wazalendo utapewa msukumo unaostahili.

4.14 Uratibu na Ushirikiano

Lengo: Kuwa na Uratibu na Ushirikiano Imara.

Kuna umuhimu kwa wadau wote kupata taarifa na takwimu kuhusu matatizo, mafanikio na mahitaji ya kissekta katika utoaji wa huduma ya maji safi na majitaka. Kukosekana kwa uratibu na ushirikiano miongoni mwa wadau husababisha migongano na miingiliano ya kiutendaji na hivyo kusababisha matumizi mabaya ya rasilimali za fedha na wataalam. Uratibu na ushirikiano baina ya wadau na vyombo vinavyotoa huduma ya majisafi na majitaka mijini utaanzishwa na kuimarishwa kwa kufanya yafuatayo:

- (i) Washikadau wakuu katika sekta wataainishwa.
- (ii) Uratibu na ushirikiano utaimarishwa na kuendelezwa.

Ramani ya Mabonde ya Mito, Tanzania

